# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI (AFISI YA RAIS) KATIBA NA UTAWALA BORA, MHESHIMIWA RAMADHAN ABDALLA SHAABANI KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NCHI (AR) KATIBA NA UTAWALA BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2006/2007

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI (AFISI YA RAIS) KATIBA NA UTAWALA BORA, MHESHIMIWA RAMADHAN ABDALLAH SHAABAN KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NCHI (AR) KATIBA NA UTAWALA BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2006/2007

## UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa likae kama Kamati ya Matumizi ili liweze kujadili na hatimae kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nchi (Afisi ya Rais) Katiba na Utawala Bora ya mwaka wa Fedha 2006/2007.

2. Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uzima na afya na kuweza kufika tena hapa leo hii kuendelea na shughuli yetu muhimu kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu. Tunaomba Mwenyezi Mungu atuzidishie hikma, busara na atupe muelekeo mwema na mashirikiano zaidi ili tuweze kufanikisha jukumu letu vizuri.

3. Mheshimiwa Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa kushinda Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Oktoba mwaka 2005 na kushika nafasi ya Urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. Kushinda kwake kumedhihirisha uwezo alionao katika kujenga umoja na kusimamia uchumi wa Zanzibar kama ambavyo Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 ilivyoelekeza. Aidha nampongeza kwa kuwa mstari wa mbele katika kuilinda amani, kudumisha utulivu uliopo na kupambana na janga la umasikini

4. Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii pia kumpongeza Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha kwa kuteuliwa tena kushika nafasi hiyo. Hii ni kutokana na utendaji mzuri na usimamizi wa siku hadi siku wa shughuli za Serikali. Pia nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Ali Juma Shamuhuna kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo. Vilevile napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa tena kushika nafasi ya Spika wa Baraza la Wawakilishi kwa kipindi kingine. Hilo ni kutokana na ufanisi na uwajibikaji wako katika kuliendesha vyema Baraza hili tukufu.

5. Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuwapongeza wajumbe wako wote kwa kuchaguliwa katika Uchaguzi Mkuu uliopita ili kuwawakilisha wananchi katika chombo hiki muhimu. Aidha nawapongeza na kuwashukuru wajumbe walioichangia hotuba ya wizara yangu katika mwaka wa fedha 2005/2006. Pongezi zangu pia nazitoa kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako tukufu chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Haji Omar Kheri, kwa ushauri, maelekezo na busara zao kwa wakati wote. Hakika michango yao imekuwa chachu kwa wizara yangu katika kutekeleza vyema majukumu yake.

6. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatoa pongezi maalum kwa wananchi wote wa visiwa vya Unguja na Pemba kwa kudumisha amani na utulivu katika nchi kwa kuonesha demokrasia ya hali ya juu iliyopelekea Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 kuwa huru na wa haki, jambo ambalo limeipa sifa nchi kitaifa na kimataifa.

7. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa nitaeleza hali halisi ya utekelezaji wa majukumu ya kazi mbalimbali ya wizara yangu katika kipindi cha mwaka 2005/2006.

## UTEKELEZAJI KWA KIPINDI CHA MWAKA 2005/2006

8. Mheshimiwa Spika, kabla sijaeleza utekelezaji wa kazi kwa kina, naomba kwanza nieleze hali halisi ya upatikanaji wa fedha kwa kipindi cha mwaka 2005/2006. Katika mwaka huo wizara yangu iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 2,772,174,000/- kwa kazi za kawaida; na shilingi 37,650,000 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2006 jumla ya shilingi 1,595,787,588.65 zilipatikana kwa kazi za kawaida ikiwa ni sawa na asilimia 57.6% ya makadirio. Kati ya hizo mishahara ilikuwa ni shilingi 1,175,631,814/- sawa na asilimia 73.7%, na shilingi 315,892,482.45 ikiwa ni sawa na asilimia 19.8% ya fedha zilizopatikana zilikuwa kwa ajili ya kuendeshea kazi. Kwa upande wa Mchango wa Serikali katika kazi za maendeleo ulikuwa ni shilingi 5,500,000/- tu ziliingizwa kati ya shilingi 18,650,000/- zilizoidhinishwa. Kwa upande wa wafadhili, wizara ilipata jumla ya shilingi 33,838,150/- kupitia Mpango wa Zanzibar wa Kupunguza Umaskini ambao ulihusu Mradi wa Kuimarisha Utawala Bora. V*iambatisho Na 1 na Na. 5 vinafafanua zaidi.*

9. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ukusanyaji wa mapato, wizara yangu katika mwaka wa 2005/2006 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 155,000,000 zitakazoingizwa katika mfuko mkuu wa Serikali. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2006, jumla ya shilingi 83,708,590/- ikiwa ni sawa na

asilimia 54% ya makadirio zilikusanywa na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. *Kiambatisho Na. 3 kinafafanua zaidi*.

10. Mheshimiwa Spika, ili kuinua elimu ya watendaji wake, katika kipindi cha mwaka 2005/2006 Wizara kupitia taasisi zake mbalimbali, imewasomesha jumla ya wafanyakazi wake 57. Kati ya hao, wafanyakazi 24 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi na 33 wanahudhuria mafunzo ya muda mrefu katika ngazi mbalimbali. *Kiambatisho Na. 6 kinafafanua zaidi.*

11. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006 jitihada za ujenzi wa misingi ya Utawala Bora ziliendelea ambapo miongoni mwao ni kwamba Mahkama imeendelea na usikilizaji wa kesi katika ngazi mbalimbali. Jumla ya kesi 5459 zilisikilizwa katika kipindi hiki na 1376 kati yake zimetolewa maamuzi. Idara ya Kuratibu Shughuli za Utawala Bora imeimarishwa kwa kupatiwa vifaa na mtaalamu. Aidha kanuni za Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zimeandaliwa. Ninayo heshima kubwa kulijuilisha Baraza lako Tukufu kuwa kazi za Ukaguzi wa Hesabu za Serikali zinaendelea vyema. Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali inaendelea na utekelezaji wa mpango wake wa kuweka taarifa zake katika mfumo wa kompyuta na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana inaendelea na mapitio ya sheria yake ili kuifanya bora zaidi. Utekelezaji wa Mpango wa kupiga vita UKIMWI unaendelea vyema chini ya Kamati Maalum ya Wizara, wakati Afisi ya Mufti, kupitia Mpango wake wa kupambana na UKIMWI kwa mbinu za Kiislamu imeleta mafanikio mazuri.

12. Mheshimiwa Spika, ninaliarifu Baraza lako tukufu kuwa hatimaye Wizara yangu imefanikisha kuanzishwa rasmi kwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka Pemba ambayo imezinduliwa rasmi tarehe 22 Februari 2006. Vile vile Wizara yangu imepata mafanikio katika mpango wake wa mashirikiano baina ya wadau wa kesi. Kwa upande mwengine, kazi ya kuanzisha kanuni kwa ajili ya mpango wa wahalifu kutumikia jamii (Community Service Programme Rules and Guidelines) imefanyika na kanuni hizo zimeanza kutumika kuanzia tarehe 1 Febuari 2006. Hali hii itapunguza msongamano wa wanafunzi (wafungwa) hasa wa makosa madogo madogo na kupelekea jamii kunufaka zaidi. Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa upande wake imeendelea vyema na kazi ya kutayarisha miswada mbalimbali ya sheria na kuishauri Serikali.

13. Mheshimiwa Spika, kumekuwa na maendeleo mazuri hivi karibuni kuhusiana na suala la Tume ya Haki za Binaadamu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufanya kazi hapa Zanzibar baada ya mazungumzo baina ya pande mbili za Muungano. Makubaliano

yaliyofikiwa ni kwa upande wa Muungano kuzingatia matakwa ya upande wa Zanzibar kwenye sheria kama ambavyo ilitakiwa na Baraza lako tukufu. Kwa upande mwingine kazi ya utoaji na uratibu wa elimu ya uraia kwa umma iliyolenga kutoa taaluma ya dhana nzima ya utawala bora iliendelea. Jumla ya vipindi vya redio 27 viliandaliwa na kurushwa hewani na Wizara. Aidha Jumuiya zisizo za kiserikali ambazo husajiliwa na Wizara zilishiriki katika kutoa elimu ya uraia na elimu ya wapiga kura hasa katika kipindi cha kuelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005.

14. Mheshimiwa Spika, ili kulinda haki za wabunifu wetu, Wizara yangu imeingia katika hatua muhimu ya kuanzisha shughuli za Afisi ya Msajili wa Hakimiliki. Afisi hii imo katika hatua za awali za kujiimarisha kwa kutafuta watendaji na vifaa vya kutendea kazi.

15. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatekeleza Mradi wa Kuimarisha Utawala Bora kupitia Mpango Mkuu wa Kupunguza Umasikini Zanzibar kwa ufadhili wa UNDP. Kupitia mradi huu, Wizara yangu imeweza kupatiwa mtaalamu, vifaa na fedha kwa ajili ya shughuli mbalimbali kama vilivyoainishwa katika Idara na taasisi mbalimbali za Wizara.

16. Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Zanzibar ilipokea ujumbe kutoka katika Umoja wa nchi za Kiafrika (AU) ulioongozwa na Profesa Adebayo Adedeji. Ujumbe huu unatoka katika Mfumo wa Nchi za Kiafrika wa Kujitathmini wenyewe (Africa Peer Review Mechanism – APRM). Ujumbe huo ulifika Tanzania Bara na Zanzibar kama hatua za awali za maandalizi ya nchi yetu kuanza taratibu za kujitathmini. Hii ni moja katika jitihada za Umoja wa Afrika chini ya mpango wa NEPAD – *New Partnership for Africa's Development* kusimamia maendeleo yao wenyewe kiuchumi, kisiasa, kijamii n.k, ikiwa ni katika jitihada za kujijenga kukabiliana na changamoto za utandawazi.

17. Mheshimiwa Spika, ILANI ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005 inatoa msisitizo wa pekee katika kuendesha Serikali kwa kufuata misingi ya Utawala Bora, kupiga vita rushwa na kufuata misingi ya haki. Suala la kuelimisha jamii kuhusu utawala bora limepewa kipaumbele na litaendelezwa katika kipindi kijacho.

18. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa nitaeleza utekelezaji halisi wa majukumu ya kazi kwa Idara na taasisi za Wizara kama ifutavyo:-.

IDARA YA UTAWALA NA UENDESHAJI

19. Mheshimiwa Spika, Idara ya Utawala na Uendeshaji ni Idara yenye jukumu kubwa la kuratibu shughuli za Wizara na kuwa ni kiungo kati ya taasisi za ndani na zile za nje ya Wizara. Aidha Idara inawajibika kutekeleza malengo inayojipangia kwa kila mwaka. Katika mwaka wa Fedha wa 2005/2006, Idara ilitekeleza malengo yafuatayo:

Kuendelea na utayarishaji wa Mpango wa Kimkakati wa Wizara *(Ministry's Strategic Plan)*

20. Mheshimiwa Spika, utayarishaji wa mpango wa kimkakakati wa Wizara umeanza kwa kutayarisha hadidu rejea kwa kazi yenyewe na kuweka bajeti ambayo imefanyika kwa ufanisi. Lengo lilikuwa ni kuifanya kazi hiyo kwa njia ya ushiriki wa pamoja kati ya wataalamu na kamati ndogo ya wafanyakazi wa Wizara. Uamuzi huo umelenga katika kukuza taaluma ya wafanyazi wa Wizara. Idara inaendelea na juhudi za kupata fedha kwa kazi hiyo ambapo maombi yake tayari yameshawasilishwa Wizara ya Fedha na Uchumi ambazo hadi sasa hazijapatikana. Jumla ya Tsh 9,000,000 zinahitajika kukamilisha kazi hiyo.

Kufanya tathmini ya kiwizara ya kazi (*job evaluation)* na hatimae kutayarisha "*job list*" na *"scheme of service:*

21. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa lengo hili haukufanikiwa kwa kiwango kilichokusudiwa, kazi imeanza kwa Idara ya Utawala na Uendeshaji tu. Katika hatua za awali imepitia na kutayarisha mapendekezo ya muundo wa Idara hii, kufuatia mabadiliko yaliyotokea baada ya kukubalika pendekezo la kuunda Idara ya Kuratibu Shughuli za Utawala Bora ambapo tayari baadhi ya vitengo vimeshahamishiwa katika Idara hii mpya. Kutokamilika kwa lengo hili kunatokana na hali iliyopo ya kuendelea na uundaji wa taasisi mbalimbali za Wizara kutokamilika.

22. Mheshimiwa Spika, mbali na malengo hayo, Idara hii pia ilifanya matengenezo ya ofisi zinazotumiwa na Idara ya Kuratibu Shughuli za Utawala Bora kwa vile Ofisi hizo ziko katika jengo la Wizara. Jumla ya shilingi 4,800,000 zilitumika kwa matengenezo hayo sawa na asilimia 68.57 ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya matengenezo ya majengo.

23. Mheshimiwa Spika, katika kuratibu kazi za Wizara Idara imeendelea kuwa ni kiungo kwa mipango yote ya Wizara na imeendelea kuratibu miradi ya maendeleo na kuratibu vikao mbalimbali vikiwemo vile vya Kamati ya Uongozi. Aidha Idara imeendelea kusimamia haki na wajibu wa wafanyakazi kwa kushajihisha utekelezaji wa majukumu na pia kwa kulinda haki zao. Katika kutekeleza hilo Idara imewapeleka masomoni wafanyakazi 5 ambao wote ni wanawake. Wafanyakazi hao wanasoma

ngazi ya cheti katika fani mbalimbali. Aidha Idara imeendelea kumsomesha mfanyakazi wake mmoja katika ngazi ya Shahada ya Uzamili katika fani Uongozi.

24. Mheshimiwa Spika, Idara hii katika kipindi cha mwaka 2005/2006 imeendelea kuwa ni msimamizi mkuu wa utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kusimamia Maadili ya Viongozi, na Idara ya Kuratibu Shughuli za Utawala Bora. Hali hii inatokana na watendaji wakuu wa Taasisi hizo kutoteuliwa rasmi.

25. Mheshimiwa Spika, pamoja na jukumu lake la kuratibu mipango ya Wizara, kusimamia haki na wajibu wa wafanyakazi, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Idara ya Utawala na Uendeshaji imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i) kuimarisha uwezo wa Idara ya Utawala na Uendeshaji katika kuratibu shughuli na kazi za Wizara;
ii) kuendelea na kazi ya utayarishaji wa mpango wa kimkakati wa Wizara ( Ministry's Strategic Plan);
iii) kutekeleza malengo ya kupambana na UKIMWI kama yalivyoelezwa katika mpango wa kimkakati wa kitaifa wa kupambana na UKIMWI chini ya usimamizi wa Tume ya UKIMWI Zanzibar;
iv) kuendelea na kazi ya kufanya tathmini ya kiwizara ya kazi (*job analysis)* na hatimae kutayarisha "*job list*"; na
v) kujenga mazingira mazuri ya kiutendaji.

26. Mheshimiwa Spika, ili Idara ya Utawala na Uendeshaji iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 291,507,000/- kwa kazi za kawaida na shilingi 19,650,000/- kwa kazi za maendeleo.

## MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA KUSIMAMIA MAADILI YA VIONGOZI

27. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kusimamia Maadili ya Viongozi ni taasisi ambayo haijasimama sawa sawa kwa kuwa uundwaji wake bado umo katika hatua za awali. Mamlaka inao baadhi ya wafanyakazi ambao wako chini ya Idara ya Utawala na Uendeshaji. Katika hatua hizo za awali za uundwaji wake Wizara ilijiwekea malengo ambayo yangepelekea kukamilisha uundwaji huo. Utekelezaji wa malengo hayo ulikuwa kama ifuatavyo:

Kukamilisha kazi ya sheria husika juu ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na kusimamia Maadili ya viongozi.

28. Mheshimiwa Spika, lengo la kukamilisha mswada wa Sheria wa kuanzisha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kusimamia Maadili ya Viongozi inaendelea kwa kufanya mashauriano ndani na nje. Mapendekezo yaliyotolewa awali yamezingatiwa kwa kuingizwa katika rasimu ya sheria hiyo. Hata hivyo Wizara imeona kuna haja ya kuzidi kuwashirikisha wahusika zaidi katika suala hilo hasa kutokana na umuhimu wake.

Kuendelea na juhudi za kuunda rasmi na kuiimarisha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kusimamia Maadili ya Viongozi

29. Mheshimiwa Spika, kuundwa rasmi kwa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kusimamia Maadili ya Viongozi kunategemea kukamilika kwa sheria yenyewe ambayo pamoja na mambo mengine itaeleza wazi mgawanyiko na majukumu ya watendaji mbalimbali wa Mamlaka hiyo sambamba na Mamlaka kuwa na nguvu za kisheria. Kwa hivyo shughuli hii haikukamilika kutokana na kutokukamilika kwa sheria husika.

Kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na mapambano juu ya kuzuia rushwa na mambo yanayohusiana nayo.

30. Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Mamlaka husika haijasimama vizuri, Wizara yangu imeendelea na utoaji wa elimu kuhusiana na kupambana na Rushwa kupitia programu ya Elimu ya Uraia. Kwa sasa utoaji wa elimu hiyo hufanyika kupitia vipindi vya redio.

31. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara yangu imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i) kuendelea na hatua za kuipitisha rasimu ya sheria husika juu ya Mamlaka;
ii) kuendelea na juhudi za kuanzisha rasmi Mamlaka inayojitegemea ya Kuzuia Rushwa na Kusimamia Maadili ya Viongozi;
iii) kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na mapambano juu ya kuzuia rushwa na mambo yanayohusiana nayo; na
iv) kupata Ofisi na Vitendea kazi kwa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na kusimamia Maadili ya Viongozi.

32. Mheshimiwa Spika, ili Wizara iweze kukamilisha uundwaji wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kusimamia Maadili ya Viongozi na kuweza kufanya kazi zake kwa ufanisi katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 75,724,099/- kwa kazi za kawaida.

IDARA YA KURATIBU SHUGHULI ZA UTAWALA BORA

33. Mheshimiwa Spika, Utawala Bora ni dhana pana ambayo inagusa maeneo mbalimbali kama vile Uchumi, Fedha, Demokrasia, Siasa na Biashara. Kuwepo kwa Idara ya Kuratibu shughuli za Utawala Bora ni muhimu katika kuhakikisha kuwa maeneo hayo yanashughulikiwa ipasavyo kwa lengo la kufikisha huduma kwa wananchi na kuleta maendeleo. Idara ya Kuratibu Shughuli za Utawala Bora ina majukumu ya kuwaunganisha wahusika wa Utawala Bora kutoka katika Taasisi za Serikali, Jumuiya zisizo za kiserikali pamoja na Sekta Binafsi. Idara hii pia ina jukumu la kusimamia na kutoa mwelekeo juu ya utekelezaji wa Utawala Bora hapa Zanzibar.

34. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa Idara ya Kuratibu Shughuli za Utawala Bora inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Wizara ilichukua hatua mbalimbali. Miongoni mwa hatua hizo ni kumwajiri Mtaalamu Mshauri (Technical Advisor) ambaye alianza kazi mwezi Septemba 2005 kwa msaada wa Shirikia la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP). Mtaalamu huyo ameajiriwa kwa utaratibu wa mkataba wa mwaka mmoja ambao unaweza kuongezwa. Katika jitahada za kuupata utaalamu wake Wizara imemteua Afisa wake mmoja kufanye nae kazi (Counterpart). Aidha baadhi ya vitengo ambavyo awali vilikuwa chini ya Idara ya Utawala na Uendeshaji vimehamishiwa katika Idara hii mpya ikiwa pamoja na wafanyakazi wake. Vitengo hivyo ni Uratibu Shughuli za Jumuiya (NGOs) na Elimu ya Uraia. Vitengo vyengine vinatarajiwa kuundwa kutegemeana na mahitaji.

35. Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Idara hii bado imo katika hatua za kuundwa kwake, imeweza kutekeleza majukumu yake kwa kiasi cha kuridhisha kama ifuatavyo:

Kupata ofisi na vitendea kazi katika Idara ya Kuratibu Shughuli za Utawala Bora

36. Mheshimiwa Spika, Idara imepata ofisi katika jengo la Makao Makuu ya Wizara kwa kuzifanyia matengenezo ofisi zilizopo ghorofa ya juu ya jengo hilo. Shughuli za matengenezo ya ofisi bado zinaendelea. Ofisi imepata vifaa kama vile kompyuta tatu, ‘printer’ moja pamoja na ‘scanner’. Aidha afisi hizo zimeungiwa mawasiliano ya “*internet*” na kuunganishwa kwa *LAN*.

Kuupitia Mpango wa Utawala Bora Zanzibar ili kufanyia kazi maeneo ambayo utekelezaji wake haujakamilika;

37. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, wizara yangu ilikusudia kuufanyia mapitio mpango wa Zanzibar wa Utawala Bora, baada ya kuwepo kwa miaka 3. Hata hivyo kutokana na kuufanyia mapitio ya Mpango Mkuu wa Kupunguza Umaskini Zanzibar (MKUZA) imebidi kazi hiyo iahirishwe ili kutoa nafasi kwa mapitio ya MKUZA kukamilika. Hali hiyo itatoa nafasi ya kuoanisha malengo na mikakati ya kiutendaji kwa mipango yote miwili.

Kuimarisha kitengo cha NGO na kuanza utekelezaji wa sera ya NGO

38. Mheshimiwa Spika, katika kukiimarisha kitengo hiki jitihada mbalimbali zimechukuliwa ili kuona kitengo kinaimarika katika utendaji wake wa kazi kwa mujibu wa Sheria ya Jumuiya (Sheria namba 6) ya mwaka 1995. Jitihada hizo ni kufanya mapitio ya majukumu ya kitengo ili kuwezesha kutayarisha muongozo, kuimarisha ushirikiano wa karibu zaidi na Afisi ya Mrajis wa Jumuiya, pamoja na kuweka mahusiano mazuri na Jumuiya zisizo za Kiserikali. Aidha hatua nyengine za kukiimarisha kitengo ni kukipatia vifaa vya kufanyia kazi sambamba na kuikamilisha sera ya Jumuiya ambayo iko katika hatua za mwisho kukamilika.

Utekelezaji wa Programu ya Elimu ya Uraia

39. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa program ya elimu ya Uraia unaendelea kwa kurusha vipindi vya redio. Mpango uliopo kwa kipindi kijacho ni kuongeza utumiaji wa mbinu nyengine zaidi za kuelimisha umma kwa kutayarisha vipindi vya televisheni, kutayarisha kijarida na kuongeza nguvu katika semina na makongamano ili kuelimisha makundi mbalimbali juu ya Utawala Bora. Katika kujiandaa na hilo Wizara imepata kifaa cha kuiwezesha kutengeneza vijarida (Print Shop Pro software).

40. Mheshimiwa Spika, pamoja na kutekeleza malengo iliyojiwekea, Idara imeweza kuwaunganisha wadau wakuu wa utawala bora, na kuweka mfumo wa kufanya kazi pamoja. Hili lilifanyika kwa kuunda kamati inayoshirikisha wawakilishi wa taasisi kuu na wahusika wa Utawala Bora. Huu ni msingi mzuri katika kuweka mfumo wa kuratibu na kutathmini Utawala Bora.

41. Mheshimiwa Spika, kupitia mashirikiano yaliyoanzishwa baina ya wahusika wa Utawala Bora, iligundulika kwamba kuna upungufu wa ujuzi katika kuandaa mipango ya utekelezaji. Idara ilitayarisha mafunzo juu ya namna ya kutayarisha mipango ya kazi (work plans) ili kuondoa upungufu huo. Mbali na jitihada hizo, pamekuwa na mawasiliano mazuri baina ya wahusika wa Utawala Bora na Wizara kwa kubadilishana uzoefu kuhusu Utawala Bora. Wizara pia imeshiriki kikamilifu katika mapitio ya Mpango wa Kupunguza Umasikini Zanzibar ambao umeiweka Sekta ya Utawala

Bora miongoni mwa maeneo makuu matatu ya mpango huo. Maeneo mengine ni Sekta ya ustawi na huduma za Kijamii na Sekta ya Kukuza Uchumi na kupunguza umaskini wa kipato. Changamoto iliyopo mbele yetu ni kuona kuwa yaliyopangwa yanatekelezwa.

42. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Idara ya Kuratibu Shughuli za Utawala Bora imejiwekea malengo yafuatayo:

i) kuelimisha makundi mbalimbali ya jamii kuhusu Utawala Bora;
ii) kujenga uwezo wa Wizara katika kupanga, kusimamia na kutathmini mageuzi ya Utawala Bora; na
iii) kuendeleza na kudumisha uhusiano wa karibu wa Wizara na wahusika wa Utawala Bora.

43. Mheshimiwa Spika, ili Idara hii ya Kuratibu Shughuli za Utawala Bora iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 54,092,000 kwa kazi za kawaida.

## MAHKAMA

44. Mheshimiwa Spika, Mahkama ni moja ya nguzo tatu za Dola kwa nchi ambayo inafuata Demokrasia na Utawala wa Sheria. Hapa Zanzibar chombo hicho cha kikatiba kinajukumu kubwa la kutafsiri sheria pamoja na kusimamia na kutoa haki kwa watu wote.

45. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Mahkama imeendelea kutekeleza malego yake kama ifuatavyo:-

### Kukarabati Majengo ya Mahkama na Kupata Vitendea Kazi

46. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006 hali ya upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida katika Mahkama ilikuwa ni asilimia 60.09 ya makadirio ya jumla ya shilingi 112,669,000/-. Kati ya fedha hizo kifungu cha ujenzi kilipata jumla ya shilingi 2,895,000/- tu hadi kumalizika mwezi wa Machi 2006. Mahkama haikuweza kuyafanyia ukarabati mkubwa majengo yake ya Unguja na Pemba kwa sababu ya ufinyu wa bajeti. Hata hivyo Mahkama imebahatika kukabidhiwa jengo lililokuwa linatumiwa na Afisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliopo Mwanakwerekwe kwa shughuli zake. Baada ya kukabidhiwa jengo hilo Mahkama ililifanyia ukarabati mdogo na hivi sasa linatumika kama Mahkama ya Kadhi wa Wilaya ya Mjini baada ya Afisi hiyo kuhamishwa katika jengo la uwanja wa Kufurahishia Watoto

Kariakoo. Hali hii imepunguza ufinyu wa nafasi uliokuwa unaikabili Mahkama hiyo.

Kuimarisha Usikilizaji na utoaji wa maamuzi katika kesi mbalimbali kwa wakati.

47. Mheshimiwa Spika, hivi sasa hakuna upungufu wa Mahakimu kwani Zanzibar ina jumla ya Mahakimu 41 wa ngazi mbalimbali ambapo Mahakimu 12 ni wa ngazi ya Mkoa, Mahakimu 14 wa ngazi ya Wilaya na 15 wa Mahkama za Mwanzo. Hali hii imepelekea huduma za usikilizaji mashauri mbalimbali kuendelea vyema katika mwaka huu wa fedha ambao umehusisha kesi za jinai na madai. Aidha mashauri ya Kiislam yaliendelea kushughulikiwa na Mahkama ya Kadhi.

48. Mheshimiwa Spika, Mahkama ya Rufaa ya Tanzania ilifanya kikao cha kusikiliza kesi za Rufaa za Zanzibar kuanzia tarehe 28 Novemba, 2005 hadi tarehe 13 Disemba, 2005 ambapo jumla ya kesi 31 zilisikilizwa. Kesi 10 kati ya hizo zilikuwa ni za Rufaa za Jinai ambazo zote zilisikilizwa na kutolewa hukumu (uamuzi). Aidha maombi matatu (3) ya Jinai (Criminal Application) yalisikilizwa na kutolewa uamuzi. Mahkama hiyo pia ilisikiliza rufaa nane (8) za Madai (Civil Appeal) ambapo zote zilitolewa hukumu. Vilevile Mahkama hiyo ilisikiliza maombi 10 ya Madai (Civil Applications) ambapo sita (6) yalitolewa uamuzi na maombi manne (4) yameakhirishwa hadi kikao kinachotarajiwa kufanyika Zanzibar mwezi Oktoba 2006. Hivi sasa kuna maombi ya rufaa za madai matatu (3) yamefunguliwa (Civil Applications) na kesi ya Rufaa ya Jinai moja (1).

49. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2005/2006 Mahkama Kuu ilipokea jumla ya kesi 14 za jinai ambazo zinaendelea. Pia ilipokea rufaa 16 ambapo 2 zimeshatolewa uamuzi na 14 zinaendelea. Kwa kesi za madai, Mahkama hiyo ilipokea kesi 43 na tayari 6 zimetolewa uamuzi na kesi 37 zinaendelea. Mahkama ilipokea Rufaa za Madai 63 na kati ya hizo 27 zimetolewa uamuzi na 36 zinaendelea. Kesi za “Probate” 214 zilipokelewa, 117 zimetolewa uamuzi na 97 zinaendelea.

50. Mheshimiwa Spika, jumla ya kesi 526 za jinai zimepokelewa katika Mahkama ya Mkoa ikiwa ni pungufu la asilimia 2.15 kulinganisha na kesi zilizopokelewa katika Mahkama hii katika kipindi kama hicho mwaka uliopita. Kati ya hizo kesi 135 zimetolewa uamuzi na kesi 391 zinaendelea. Kwa upande wa kesi za madai zilipokelewa ni 38 na kati ya hizo 6 zimetolewa uamuzi na 32 bado zinaendelea. Rufaa 32 za jinai zimefunguliwa 14 zimetolewa uamuzi na 18 bado zinaendelea. Aidha Rufaa za Madai 442 zilifunguliwa. Kati ya hizo 378 zimetolewa uamuzi na 64 zinaendelea.

51. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi wa Februari, Mahkama ya Wilaya imepokea jumla ya kesi 3024 za jinai ikiwa ni ongezeko kwa asilimia 4.1 kulinganisha na mwaka uliopita. Kesi za madai 56 zilifunguliwa 8 zilitolewa uamuzi 48 zinaendelea. Rufaa za madai 16 zimefunguliwa.

52. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi wa Machi, 2005 hadi kufikia Februari 2006 Mahkama ya Mwanzo imepokea jumla ya kesi 1,382 za jinai ikiwa ni pungufu la asilimia 16.18 ya kesi zilizopokelewa mwaka uliopita. Kati ya hizo 772 zimetolewa uamuzi na 610 zinaendelea. Aidha Mahkama hii imepokea kesi 300 za madai ikiwa ni pungufu la asilimia 0.21 ya kesi za aina hii zilizopokelewa mwaka uliopita. Kesi 120 zimetolewa uamuzi na 180 zinaendelea.

53. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Februari, 2006 Mahkama ya Kadhi imepokea jumla ya kesi 837 katika ngazi ya Wilaya ikiwa ni ongezeko la asilimia 0.99 ya ile idadi ya kesi zilizofunguliwa katika kipindi kama hicho cha mwaka uliopita. Kati ya hizo, kesi 608 zimetolewa uamuzi na 229 zinaendelea. Mahkama ya Kadhi wa Rufaa imepokea rufaa 30 ikiwa ni ongezeko kwa asilimia 0.02 Katika kipindi kama hiki mwaka uliopita kati ya kesi hizo 22 ziliweza kutolewa uamuzi. Kwa upande wa Mahkama ya Watoto jumla ya kesi za jinai 73 zimepokelewa na hii ni sawa na upungufu wa asilimia 0.5 ya kesi zilizopokelewa katika kipindi kama hicho mwaka uliopita. Kati ya kesi hizo 26 zimetolewa uamuzi na 47 zinaendelea.

## Kuwaendeleza Wafanyakazi Kielimu

54. Mheshimiwa Spika, ufanisi wa kazi za Mahkama unahitaji wafanyakazi wake kuwa na kiwango kizuri cha elimu ili kumudu vyema majukumu mbalimbali na ndio maana imekua ikitilia mkazo suala hilo kwa kuwaendeleza wafanyakazi wake wa kada mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 Mahkama iliendelea na jukumu lake la kuwapatia wafanyakazi wake taaluma mpya. Katika hilo jumla wafanyakazi 3 wamepata mafunzo ya muda mrefu katika vyuo mbalimbali ambapo kati yao wafanyakazi 2 wanawake wanasoma Stashahada. Mfanyakazi mmoja mwanamme anasoma Shahada ya Uzamili. Mbali ya wafanyakazi hao wapya kupatiwa mafunzo Mahkama imekuwa ikiwahudumia wafanyakazi wake 4 ambao bado wanaendelea na masomo ambayo walianza katika miaka ya nyuma. Katika kipindi cha 2005/2006 jumla ya wanafunzi 3 wamemaliza masomo na kuripoti kazi.

55. Mheshimiwa Spika, kufikia mwezi Machi, 2006 jumla ya semina tatu zilifanyika, mbili kati yao zilikua kwa ajili ya Makarani wa Mahkama ambapo moja ilifanyika Unguja na nyengine Pemba. Semina ya Makarani wa Unguja ilifanyika katika ukumbi wa Bwawani kuanzia tarehe 27 Julai na 28 Julai 2005 ambayo iliendeshwa na wakufunzi kutoka Chuo cha Uongozi wa Mahkama. Kadhalika semina ya Makarani wa Pemba ilifanyika katika ukumbi wa Makonyo Chakechake Pemba. Lengo la semina hizo ni kuwapatia mbinu mbalimbali Makarani juu ya kushughulikia utayarishaji wa mashauri ili kusaidia upunguzaji na ucheleweshaji wa mashauri. Semina hizo zilighariimu shilingi 15,975,000/-

56. Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio iliyopata Mahkama katika kipindi cha 2005/2006 bado imekabiliwa na matatizo kadhaa. Majengo mengi yanayotumika ni yale yaliyorithiwa tokea enzi za ukoloni ambayo yamechakaa, uhaba wa upatikanaji wa fedha kulingana na bajeti husika na upungufu wa nyenzo za kufanyia kazi. Mrundikano wa mashauri ya aina mbalimbali pamoja na wafanyakazi wake wengi wa ngazi ya ukarani kutokuwa na elimu ya kutosha.

57. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi wa Februari, 2006 Mahkama imeweza kukusanya jumla ya shilingi 10,554,585/-/- kati ya lengo lililowekwa la kukusanya shilingi 32,500,000/-. Ukusanyaji huo ni sawa na asilimia 32.48 ya makadirio yaliyowekwa. Hali hiyo ya ukusanyaji mdogo imechangiwa na kutokamilika kwa kesi kunakosababishwa na kukosekana kwa fedha za kuwalipa mashahidi. Aidha katika mwaka wa fedha 2006/2007 Mahkama imejiwekea lengo la kukusanya na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali jumla ya shilingi 35,000,000/-.

58. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2006/2007 Mahkama imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i) kufanyia matengenezo Mahkama za Unguja na Pemba;
ii) kuimarisha usikilizaji na utoaji wa maamuzi katika kesi mbalimbali kwa wakati;
iii) kuwaendeleza wafanyakazi kielimu;
iv) kuanzisha Chama cha Majaji na Mahakimu, Zanzibar; na
v) kupitia upya mfumo wa usimamizi wa Mahkama za Watoto.

59. Mheshimiwa Spika, ili Mahkama iweze kutekeleza malengo yake iliyojipangia kwa mwaka 2006/2007, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 849,000,000/- kwa kazi za kawaida.

AFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

60. Mheshimiwa Spika, Afisi ya Mwanasheria Mkuu ina majukumu makuu mawili ambayo yameainishwa katika kifungu cha 56 cha Katiba ya Zanzibar ambayo ni kuwa Mshauri Mkuu wa kisheria kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kutekeleza shughuli nyengine zozote za kisheria zitakazo agizwa na Rais au kwa mujibu wa maelekezo ya Katiba au Sheria nyingine zozote. Jukumu jengine muhimu la Afisi ya Mwanasheria Mkuu ni la uandishi wa Miswada ya Sheria za Serikali. Katika mwaka wa fedha wa 2005/2006 jumla ya Miswada ya Sheria 7 ilitayarishwa na kuwasilishwa Barazani; hii ikiwa ni upungufu asilimia 75 ikilinganishwa na mwaka 2004/2005. Miswada ya sheria hizo husika ni kama ifuatavyo:

i. Sheria ya Makisio ya mwaka, 2005.
ii. Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato ya Serikali) ya 2005.
iii. Sheria ya Rufaa za Kodi Zanzibar, 2006.
iv. Sheria ya Vyakula, Madawa na Vipodozi ya Zanzibar, 2006.
v. Sheria ya Shirika la Umeme Zanzibar, 2006.
vi. Sheria ya Maji, 2006.
vii. Sheria ya Usafiri wa Baharini, 2006.

61. Mheshimiwa Spika, vilevile Afisi ya Mwanasheria Mkuu inajukumu la kuandika Sheria ndogo ndogo (By-Laws) pamoja na Hati mbalimbali za kisheria (Legal Notices) kutoka Wizara na Idara za Serikali. Katika mwaka wa fedha wa 2005/2006, Afisi ya Mwanasheria Mkuu iliweza kuandika jumla ya Sheria ndogo ndogo na Hati za Kisheria 70.

62. Mheshimiwa Spika, aidha Afisi ya Mwanasheria Mkuu ina jukumu la kuiwakilisha Serikali Mahakamani katika Kesi zote za Hukukia (Civil Litigations) zinazoihusisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Katika mwaka wa fedha 2005 / 2006 jumla ya Kesi za Hukukia 19 zilisimamiwa katika Mahkama Kuu ya Zanzibar pamoja na Mahkama ya Rufaa ya Tanzania, hapa Zanzibar. Hili ni Upungufu la kiasi 13% ikilinganishwa na mwaka 2005 / 2006 ambapo kulikuwa na Kesi 22.

63. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2005/2006 Afisi ya Mwanasheria Mkuu imeendelea na jukumu lake la kuishauri Serikali na vyombo vyake katika mambo ya sheria. Aidha Wanasheria wake wameweza kushirikiana na Kamati mbalimbali za Serikali na Kamati za Baraza la Wawakilishi hasa wakati wa kuipitia Miswada ya Sheria kabla ya kuwasilishwa katika Baraza lako tukufu. Vile vile Afisi imepokea malalamiko mbalimbali kutoka kwa wananchi dhidi ya baadhi ya vyombo

vya Serikali yanayohusiana na utekelezaji wa Sheria na kushauriwa ipasavyo.

64. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2005 / 2006 Afisi ya Mwanasheria Mkuu, iliendelea na utekelezaji wa kazi, majukumu na malengo yake kwa kiwango cha kuridhisha. Serikali iliendelea kushauriwa kwa hekima na busara kwa kufuata maelekezo na masharti ya Katiba pamoja na sheria nyingine mbalimbali; jambo ambalo limesaidia kuimarisha Utawala Bora na kujenga mshikimano utulivu na amani katika nchi yetu. Mbali na hayo Afisi imeweza kutekeleza mambo yafuatayo:-

Kuwapatia elimu ya ziada wafanyakazi wa kada mbalimbali

65. Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuwaendeleza wafanyakazi wake katika mwaka 2005/2006, jumla ya wafanyakazi 12 wamepatiwa elimu ya ziada ambapo Wanaume ni saba na Wanawake ni watano. Kati ya hao wafanyakazi wawili (2) wamesomea "Legislative Drafting" huko Marekani kwa msaada wa UNDP. Mfanyakazi mmoja amesomea "Legislative Drafting" Ghana kwa msaada wa *Common Wealth Secretariate* na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Wafanyakazi 7 wamesomea "Civil Litigation - Techniques" wakati Wafanyakazi wawili wamefanya mafunzo ya "DataBase" kwa msaada wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa (UNDP).

Kuzidisha juhudi ya kupata vifaa vya kufanyia kazi, ikiwa ni pamoja na huduma za usafiri

66. Mheshimiwa Spika, lengo la kupata vifaa vya kufanyia kazi (ikiwa ni pamoja na huduma za usafiri) limeweza kutekelezwa nusu kwa kupatiwa gari mpya Mwanasheria Mkuu. Vifaa vingine vya kazi havikuweza kupatikana kutokana na ukosefu wa fedha.

Kuendelea na utoaji wa mafunzo ya vitendo kwa wanasheria wapya wa taasisi mbalimbali za Serikali

67. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006 jumla ya Wanasheria wapya tisa (9) (Wanawake 4 na Wanaume 5) wamepokelewa kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali kwa ajili ya kupatiwa mafunzo ya vitendo (Internship Programme). Bado wanasheria hao wanaendelea na mafunzo hayo.

Kuimarisha Tume ya Kuchunguza Sheria

68. Mheshimiwa Spika, katika uimarishaji wa Tume ya Kuchunguza Sheria, Afisi imewaajiri wanasheria 2 wapya. Tume hiyo sasa ina jumla ya wanasheria 4 pamoja na Mwenyekiti. Afisi pia imeweza kuipatia Tume hiyo seti moja ya kompyuta pamoja na vifaa vyake. Tume imekabidhiwa

Jengo Kongwe liliopo ndani ya Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora ili lilifanyie ukarabati na kuweza kulitumia kwa matumizi ya Ofisi ya kudumu. Kiasi cha shilingi 10,000,000/- zitahitajika kwa ukarabati wa jengo hilo.

Kuchapisha sheria kwa kushirikiana na kampuni ya LAW AFRICA PUBLISHING LIMITED

69. Mheshimiwa Spika, lengo la kuchapisha vitabu vya sheria halijaweza kutekelezwa kutokana na kampuni ya Law Africa Publishing Limited kutokuonesha hamu ya kuendeleza mradi huu. Katika jitihada za kuhakikisha kwamba utekelezaji wa lengo hili haukwami, Afisi hii imewasiliana na Shirika la Maendeleo la Kimataifa (UNDP) ili kuangalia uwezekano wa kusaidia. Baada ya mawasiliano Shirika hilo limeahidi kusaidia jumla ya dola 10,000 katika mwaka wa fedha wa 2006/2007.

70. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 pamoja na kuendelea kutekeleza kazi na majukumu ya kimsingi, Afisi ya Mwanasheria Mkuu inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo -

i) kuwapatia elimu ya ziada (kwa lengo la kujenga “specialization”) wafanyakazi wa kada mbalimbali;
ii) kuendeleza juhudi za kuanzisha Maktaba ya vitabu vya Sheria kwa mashirikiano na Asasi nyingine za Sheria kama vile Mahkama Kuu na kadhalika;
iii) kutafuta nyezo kwa ajili ya upanuzi wa Afisi
iv) kuendeleza uimarishaji wa Tume ya Kuchunguza Sheria; na
v) kuendeleza juhudi za kutekeleza mpango wa uchapishaji wa vitabu vya Sheria za Zanzibar.

71. Mheshimiwa Spika, ili Afisi ya Mwanasheria Mkuu iweze kutekeleza malengo yake iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2006/2007 naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 336,563,000/- kwa matumizi ya kawaida.

AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

72. Mheshimiwa Spika, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka sasa inatimiza miaka minne tokea kuanzishwa kwake mwaka 2002 kufuatia marekebisho ya nane ya Katiba ya Zanzibar. Majukumu, uwezo na mamlaka iliyonayo Afisi hii yamewekwa bayana katika kifungu namba 56A (1) hadi (10) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na Sheria ya Nyendo za Jinai Nambari 7 ya mwaka 2004.

73. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iliendelea kutekeleza shughuli zake za kazi za kawaida na kusimamia utekelezaji wa malengo iliyojiwekea. Kwa upande wa utekelezaji wa kazi za kawaida ambazo zinajumuisha uendeshaji wa kesi na kutoa ushauri kwa jeshi la Polisi juu ya upelelezi wa kesi mbalimbali jumla ya majalada 278 yamepokelewa na ofisi na kufanyiwa kazi katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2005 hadi Machi 2006. Aidha kesi 15 zimefunguliwa katika Mahkama Kuu na kesi 12 zimesimamiwa katika Mahkama ya Rufaa Tanzania. Kesi nyengine zilizofunguliwa katika Mahkama za Mikoa - Vuga 218 Mwera 69, Mfenesini 71 na 39 kwa Mahkama za Mikoa Pemba. Kwa upande wa malalamiko, Afisi imepokea jumla ya malalamiko 79 kutoka kwa wananchi mbalimbali kuhusiana na uendeshaji wa kesi za jinai. Kwa kushirikiana na Polisi na Mahkama Afisi imeweza kuyashughulikia malalamiko hayo. Kwa upande wa malengo iliyojiwekea katika mwaka huu unaomalizika wa 2005/2006 utekelezaji wake ulikuwa kama ifuatavyo:

## Kuimarisha jengo kwa ajili ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba

74. Mheshimiwa Spika, hatua za kulifanyia matengenezo jengo lililopo sehemu ya chini ya jengo la Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora hapo Chakechake zilikwenda kama ilivyopangwa na kukamilika mwishoni mwa mwaka 2005. Aidha vifaa vyote muhimu kwa uendeshaji wa ofisi vimeshawekwa ikiwa ni pamoja na kompyuta, mashine ya 'photocopy' huduma za simu na gari moja ndogo kwa usafiri wa ofisini. Hatua za ufungaji wa mawasiliano ya 'internet' zimeanza kuchukuliwa na zinatarajiwa kukamilika kabla ya kumalizika kwa mwaka huu wa fedha. Mwanasheria mmoja tayari amepelekwa Pemba na ofisi sasa inafanya kazi baada ya kuzinduliwa rasmi hapo tarehe 22 Febuari, 2006.

## Kukamilisha taratibu kwa Wanasheria wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kuendesha mashtaka katika Mahkama za Mikoa Pemba.

75. Mheshimiwa Spika, Kufikiwa kwa lengo hili kulitegemea zaidi kukamilika kwa uimarishaji Afisi – Pemba pamoja na kupatiwa nyenzo za kufanyia kazi. Kwa kuwa matayarisho ya kuanza kazi kwa ofisi yamekamilika, tayari sasa kesi katika Mahkama zote mbili za Mikoa zinaendeshwa na mwanasheria kutoka Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Kuanza kazi kwa Afisi ya Pemba kunahitimisha awamu ya kwanza ya kuendesha kesi katika Mahkama zote za Mikoa ya Unguja na Pemba.

## Kuwapatia mafunzo wanasheria na watendaji wengine

76. Mheshimiwa Spika, Afisi iliendelea na juhudi zake za kuwatafutia na kuwashajihisha wafanyakazi wake kutafuta nafasi za kujiendeleza zaidi

kielimu. Katika mwaka wa 2005/2006, mfanyakazi mmoja amerudi mafunzoni baada ya kuhitimu mafunzo ya mwaka mmoja ya Utawala katika kiwango cha Stashahada ya Uzamili na mfanyakazi mmoja anaendelea na mafunzo ya Stashahada ya Sheria. Aidha wafanyakazi wanne wamemaliza mafunzo ya vitendo ya miezi 3 huko Mahkama ya Kimataifa ya Rwanda (ICTR) Arusha na wengine wawili wameanza mafunzo kama hayo katika mwezi wa April 2006. Mafunzo haya yana umuhimu wa pekee kwa vile huwapatia washiriki uzoefu wa kimataifa katika uendeshaji wa kesi hasa zinazohusiana na mauaji. Mfanyakazi mmoja amehudhuria mafunzo mafupi ya Uongozi wa Fedha nchini Swaziland. Aidha yametolewa mafunzo ya wiki moja kwa wanasheria wote wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka juu ya uendeshaji bora wa mashtaka.

## Kuchapisha na kusambaza Mwongozo wa Uendeshaji wa Mashtaka kwa Wahusika

77. Mheshimiwa Spika, Kazi ya kutayarisha mwongozo huo ilifanyika kwa ufanisi baada ya kuajri mshauri kutoka Kitivo cha sheria cha Chuo Kikuu Dar es salaam. Aidha mwongozo huo umechapishwa na tayari umeanza kutumika baada ya kusambazwa kwa wadau mbalimbali wa sheria

## Kuendeleza mpango wa pamoja wa mashirikiano

78. Mheshimiwa Spika, Mafanikio yoyote ambayo ofisi hii inaweza ikayapata yanatokana na mashirikiano makubwa inayoyapata kutoka katika vyombo mbalimbali vinavyosimamia sheria. Vyombo hivyo ni pamoja na Mahkama, Chuo cha Mafunzo na Jeshi la Polisi. Katika kuhakikisha kuwa mashirikiano hayo yanaimarika, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imeanzisha utaratibu wa vikao vya pamoja vya kila robo mwaka na kile cha mwisho wa mwaka kwa lengo la kutathmini utendaji wetu na kujadili mikakati mbalimbali ambayo inaweza ikasaidia kuleta ufanisi wa kazi.

79. Mheshimiwa Spika, Afisi pia iliandaa mafunzo juu ya usimamizi wa uendeshaji wa kesi za jinai yaliyowashirikisha Majaji, Wanasheria wa ofisi hii, Mahakimu wa Mikoa, wawakilishi kutoka Idara ya Mazingira, Manispaa na Jumuiya ya Wanasheria Zanzibar wakiwa ndio wadau wakuu katika masuala ya kesi za jinai nchini. Mafunzo hayo yalilenga katika usimamiaji bora wa kesi za jinai ili kupunguza matumizi mabaya ya vyombo vya Sheria na kuhakikisha usikilizaji haraka wa kesi. Aidha Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iliaandaa semina kwa vyombo vya habari juu ya taratibu za uandishi wa taarifa zinazohusu kesi za jinai.

Kuanzisha kanuni kwa ajili ya mpango wa wahalifu kutumikia jamii (Community Service Programme Rules and Guidelines)

80. Mheshimiwa Spika, Baraza lako tukufu bado linakumbuka marekebisho ya Sheria ya Nyendo za Jinai nambari 7 ya 2004. Sheria hiyo ilitamka bayana kuwa kutakuwa na adhabu za kutumikia jamii kwa wakosaji watakaotiwa hatiani kwa makosa madogo ambayo adhabu yake ni kifungu kisichozidi miaka miwili. Hata hivyo kuanza kutumika kwa adhabu hizo kulitakiwa kufatie kutungwa kwa kanuni zitakazoweka utaratibu unaokubalika wa mpango wa kutumikia jamii 'community services programme Rules and Guidelines'. Nina furaha kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa Kanuni hizo tayari zimetayarishwa, zimeshachapishwa na zimeanza kutumika kuanzia tarehe 1 Febuari 2005. Wadau mbalimbali wakiwemo Wakurugenzi wa Maidara yahusianayo na jamii, Mahakimu ngazi zote pamoja na Majaji, Chuo Cha Mafunzo, Jeshi la Polisi na Wanasheria katika Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka wamepatiwa mafunzo juu ya matumizi ya Kanuni hizo.

Kuimarisha Maktaba kwa kuanza ujenzi wa jengo maalum la maktaba na kupata vitabu zaidi

81. Mheshimiwa Spika, Uimarishaji wa huduma za maktaba ni moja kati ya malengo ya muda mrefu katika Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Hii inatokana na kukuwa kwa mahitaji ya huduma hizo yanayojitokeza kila siku. Maktaba iliyopo sasa ambayo haikidhi haja kwa nafasi pamoja na machapisho mbalimbali inaendelela kujipatia umaarufu kutokana na ongezeko la watumiaji wa huduma zinazotolewa. Majaji, Mahakimu na wadau wengine wa sheria wamekuwa wakiitumia maktaba hii kwa ajili ya kufanyia rejea. Rejea hizo inajumuisha vitabu vya sheria (text books) pamoja na vitabu vya kesi za miaka iliyopita (Law Reports). Aidha, wanafunzi wa vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi wamekuwa wakifika ofisini kutumia huduma za maktaba ama kwa kufanya rejea za masomo yao au kukamilisha ripoti za tafiti zao mbalimbali wanazozifanya.

82. Mheshimiwa Spika, katika kufanikisha azma ya kuwa na jengo maalumu la maktaba, ofisi imefanya juhudi mbalimbali za kutafuta fedha za kugharamia ujenzi huo. Nina furaha kuliarifu baraza lako tukufu kuwa Benki ya Maendelo ya Afrika (ADB) imekubali kutoa kiasi cha fedha kugharamia mradi huu.

83. Mheshimiwa Spika, pamoja na kutekeleza majukumu yake kwa kutimiza malengo yake kwa kiwango cha kuridhisha, Afisi hii bado imekuwa ikikabiliwa na tatizo la kutopatikana fedha za kuendeshea kazi zikiwemo fedha kwa mahitaji ya umeme, maji, huduma za simu na mafuta ya magari. Tatizo jengine linaloikabili Afisi hii ni uhaba wa ofisi na samani

hasa pale awamu ya pili ya uendeshaji mashtaka katika Mahkama za wilaya itakapoanza katika mwaka ujao wa fedha.

84. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2005 hadi Machi 2006 Afisi iliweza kupata jumla ya shilingi 112,865,090/- sawa na asilimia (54%) ya fedha zilizoombwa na kuidhinishwa ambazo ni shilingi 204,000,000/-. Kati ya fedha hizo zilizopatikana, shilingi 77,837,436/- sawa na asilimia sabiini (70%) zimetumika kwa ajili ya mishahara na marupurupu ya wafanyakazi na shilingi 35,027,654/- zimetumika kwa matumizi mengineo ya kuendesha Afisi, ambapo kati yake shilingi 15,500,000/- zimetumika kwa matengenezo ya jengo la Afisi huko Pemba.

85. Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wafadhili jumla ya shilingi 91,450,226/- zilitolewa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa UNDP katika kipindi cha Julai 2005 hadi Machi 2006. Pesa hizo ziligharamia mafunzo ya vitendo kwa wanasheria, mafunzo mafupi, ununuzi wa vitendea kazi kwa Afisi ya Pemba. Pia viligharamia mafunzo kwa Wanasheria juu ya *Forensic Evidence,* mafunzo kwa waandishi wa habari juu ya uandishi wa habari zinazohusu mambo ya jinai, mkutano wa tathmini wa wadau wa Sheria, kuajiri mshauri wa kutayarisha "*Criminal Procedure Rules"* na utayarishaji wa Kanuni za mpango wa kutumikia jamii na kuzichapisha. Kupatikana kwa msaada huu kumeisaidia kwa kiasi kikubwa Afisi hii kufanikisha utekelezaji wa malengo iliyojiwekea.

86. Mheshimiwa Spika, katika kipindi kijacho cha mwaka wa fedha 2006/2007, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka itaendelea na utekelezaji wa kazi zake za kila siku kama ilivyoainishwa ndani ya Katiba ya Zanzibar na Sheria mbalimbali. Aidha Afisi imepanga malengo maalumu yafuatayo, ambayo inatarajia kuyakamilisha katika mwaka ujao wa fedha.

i) kuanza matayarisho ya uendeshaji mashtaka Mahkama za Wilaya. Utekelezaji wa lengo hili utajumuisha ujenzi wa jengo la ziada la ofisi, upatikanaji wa vitendea kazi, uajiri wa Wanasheria wa ziada na mafunzo kwa Mahakimu na Waendesha Mashtaka wa ngazi za Wilaya;
ii) kuendelea kuwapatia mafunzo wanasheria na watendaji wengine wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka katika kuhakikisha utendaji bora wa kazi zao za kila siku;
iii) kuendeleza mpango wa pamoja wa mashirikiano kati ya Mahkama, Chuo cha Mafunzo, Jeshi la Polisi na Afisi yetu katika mpango wa usimamiaji kesi za jinai na hatimae kuharakisha uendeshaji bora wa mashtaka;
iv) kuimarisha Maktaba kwa kuanza ujenzi wa jengo maalum la maktaba na kupata vitabu zaidi;

v) kuanzisha mpango maalum wa kuelimisha jamii mambo yanayohusu mashtaka ya jinai kwa njia ya kumbukumbu za kudumu; na
vi) kuanzisha (data base) ya kesi za jinai na mienendo yake.

87. Mheshimiwa Spika, kwa kuiwezesha Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kutekeleza kazi iliyojipangia katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007 – naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Shillingi 606,200,000/- kati ya hizo shilingi 371,000,000/- kwa kazi za kawaida na shilingi 196,000,000/- kwa kazi za maendeleo.

## AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

88. Mheshimiwa Spika, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni taasisi muhimu katika kuimarisha misingi ya Utawala Bora kama ilivyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020 pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005. Katika kipindi cha 2005/2006 Afisi imeendelea kufanya kazi zake kwa mujibu wa katiba ya Zanzibar kifungu No.112(3) ya mwaka 1984 na kwa mujibu wa sheria ya kuanzishwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, sheria namba 11 ya mwaka 2003. Jukumu kubwa la Afisi hii ni kuzifanyia ukaguzi fedha zote zinazotolewa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali na kutoa taarifa zake za ukaguzi katika Baraza la Wawakilishi.

89. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006. Afisi imekamilisha Ripoti ya ukaguzi wa mahesabu ya mwaka 2002/2003 na tayari ripoti hiyo imeshawasilishwa katika Baraza lako tukufu ili ipate kufanyiwa kazi na Kamati ya kuchunguza Mahesabu ya Serikali (PAC).
Vilevile matayarisho ya kitabu cha ripoti ya mahesabu kwa kipindi cha mwaka 2003/2004 yameshakamilika .

90. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kazi za ukaguzi wa mahesabu ya mwaka 2004/2005, katika taasisi mbalimbali za serikali zimekamilika na taarifa za ukaguzi huo zimeshawasilishwa katika taasisi zinazohusika kwa kufanyiwa kazi, mara tu majibu ya hoja za ukaguzi huo yatakapokamilika kazi za utayarishaji wa kitabu cha ripoti za mwaka huo zitaanza. Vilevile kazi ya ukaguzi wa mahesabu kwa kipindi cha mwaka 2005/2006 zimeshaanza kwa baadhi ya taasisi za Serikali na inatarajiwa kazi hiyo itamalizika kwa wakati muafaka na hatimae ripoti yake itawasilishwa kunakohusika kwa mujibu wa sheria zilizopo. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006 Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar iliweza kutekeleza malengo yaliyojiwekea kama ifuatavyo:-

Kuendelea na Ukaguzi katika Halmashauri za Wilaya na kuziimarisha Ofisi zilizomo Mikoani

91. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2005/2006 Afisi hii iliendelea na ukaguzi wa mahesabu katika Halmashauri za Wilaya ikiwa ni sehemu ya kazi zake za kawaida. Ukaguzi katika Halmashauri za Wilaya unaoendelea umeleta mafanikio mazuri katika uimarishaji na uwekaji wa kumbukumbu katika Halmashauri hizo. Watendaji wa Halmashauri hizo wameweza kupata taaluma jinsi ya kuweka vitabu na kumbukumbu nyengine za mahesabu, ambapo kumekuwa na tafauti kubwa ya hoja zilizotolewa katika kipindi cha mwaka 2003/2004 na mwaka 2004/2005. Taarifa za ukaguzi tayari zimeshawasilishwa katika Halmashauri husika na matarajio ya Afisi kuwa taarifa hizo zitakuwemo katika ripoti ya mwaka 2003/2004.

Kuendelea na kujenga uwezo wa Afisi na watendaji

92. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2005|2006 Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu iliendelea na jitihada zake za kuwandeleza kitaaluma wafanyakazi wake kwa kuwapatia mafunzo yanayohusiana na Kada ya Uhasibu na Ukaguzi ya muda mrefu na mfupi hapa nchini. Katika hilo jumla ya wafanyakazi 10 wamepelekwa masomoni kwa ajili ya mafunzo ya muda mrefu yakiwemo shahada ya uzamili “Post graduate diploma”, stashahada ya juu “Advanced Diploma”, stashahada “Ordinary Diploma” na Cheti “Certificate”. *Kama Kiambatisho Na 6 (A) kinavyoonesha*.

93. Mheshimiwa Spika, Afisi imeweza kuhamasisha wafanyakazi wake kujiunga na Bodi ya Wahasibu na wakaguzi ya Tanzania na kuweza kupata nafasi ya kufanya mitihani inayoandaliwa na Bodi hiyo ili kuweza kuendeleza viwango vya elimu katika fani ya uhasibu na ukaguzi. Jumla ya wafanyakazi 12 ambao wamehitimu na kupata diploma (Advanced Diploma in accountancy na Diploma ya juu uzamili) wameshasajiliwa kufanya mihani ya bodi hiyo

94. Mheshimiwa Spika, vilevile mafunzo mbalimbali ya muda mfupi yametolewa na Afisi kupitia mradi wa uimarishaji wa Afisi kwa wafanyakazi katika viwango tofauti. Wafanyakazi 21 ambao wameajiriwa katika kipindi cha mwaka 2004/2005 walipatiwa mafunzo ya awali ya ukaguzi wa hesabu kati ya hao 17 ni wanaume na 4 wanawake. Aidha wafanyakazi 30 wa ngazi ya utendaji walipata mafunzo yanayohusiana na kazi za ukaguzi wa Miradi inayofadhiliwa na wahisani. Pamoja na mafunzo ya awali ya mfumo mpya wa malipo unaotumiwa na Serikali.

Kukamilisha Kanuni mbalimbali za utekelezaji wa sheria Namba 11 ya mwaka 2003 zitakazoipa nguvu sheria hiyo.

95. Mheshimiwa Spika, hatua ya kufanikisha kanuni mbalimbali za utekelezaji wa Sheria Namba 11 ya mwaka 2003 imeshakamilika Ni matumaini yetu kuwa kanuni hizo zitaanza kutumika wakati wowote mara taratibu husika zitakapokamilika.

96. Mheshimiwa Spika, mbali na malengo niliyokwisha kuyaainisha hapo juu vilevile Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu imeweza kufanikisha uhusiano mzuri uliopo kati yake na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kiwango kikubwa kabisa. Mashirikiano hayo yameweza kuzaa matunda mazuri na kuweka muelekeo mzuri katika kuendelea kwa Afisi hii. Lengo kuu ni kuendeleza mashirikiano yaliyopo kati ya Afisi zetu hizi mbili na kuhakikisha kwamba Afisi yetu inakwenda sambamba na mabadiliko mbalimbali yanayotokana na kasi ya maendeleo ya Sayansi na Tekenolojia ili kuweza kukabiliana na athari za mabadiliko hayo.

97. Mheshimiwa Spika, kupitia mashirikiano hayo Afisi imeweza kupata nafasi za kushiriki kikamilifu katika shughuli za kitaifa na kimataifa pale ambapo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inapopata ushiriki katika maeneo mbalimbali ikiwemo mikutano, makongamano n.k. Miongoni mwa mambo machache ambapo Afisi ilishirikiana vyema katika kipindi cha 2005/2006 ni kupata nafasi ya kushiriki katika mkutano mkuu wa Kimataifa uliohusisha Wakaguzi Wakuu wa Mahesabu wa nchi za Afrika zinazozungumza Kiengereza (AFROSAI-E) uliofanyika mwezi Machi 2006 ambapo Tanzania ilikua mwenyeji wa mkutano huo. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar pamoja na Maofisa 2 wa ngazi ya juu walishiriki katika Mkutano huo.

98. Mheshimiwa Spika, sambamba na mkutano huo, Afisi iliweza kuhudhuria katika kongamano linalohusu utendaji wa kazi za ukaguzi kwa nchi mbalimbali zilizomo katika jumuia ya AFROSAI-E ambapo mikakati mbalimbali iliwekwa ili kuweza kufanikisha kazi za ukaguzi katika nchi hizo.

99. Mheshimiwa Spika, Afisi imeweza kufanya kazi za ukaguzi wa hesabu katika miradi mbalimbali kwa kushirikiana na wafanyakazi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa yale maeneo ambayo mashirika yalipaswa kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Tanzania na kutoa ripoti ya pamoja. Aidha mazungumzo ya awali yameshaanza

kufanyika kuhusu kufanya ukaguzi katika Taasisi za Muungano zilizopo Zanzibar.

100. Mheshimiwa Spika, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeweza kukusanya jumla ya Shillingi 1,890,000/- hadi kufikia Machi 2006 sawa na asilimia 75.6% ya makadirio. Katika kipindi cha 2006/2007 Afisi hii imekusudia kukusanya na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali jumla ya Shillingi 3,000,000/-

101. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2006/2007 Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i) kufanya ukaguzi katika taasisi zote za Serikali na kutoa taarifa za ukaguzi huo kwa wakati na kwa mujibu wa sheria zilizopo
ii) kufanya ukaguzi yakinifu (Value For Money Audit) kwa maeneo yatakayo chaguliwa kulingana na upatikanaji wa nyezo za kufanyia kazi;
iii) kuwaendeleza wafanyakazi wake kitaaluma kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu, ndani na nje ya nchi.
iv) kuendelea kujenga uhusiano na mashirikiano yaliyoanzishwa kati ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;
v) kuziimarisha Afisi zake zilizopo Mikoani kwa kuzipatia vitendea kazi vya kisasa; na
vi) kujiunga katika jumuia za kimataifa ili kuweza kupata nafasi za masomo na nyaraka mbalimbali zinazotolewa na jumuia hizo kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kazi zetu. Mfano SADCO –SAI, AFROSAI-E na INTOSAI.

102. Mheshimiwa Spika, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili iweze kutekeleza malengo ya kazi zake kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2006/2007 naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shillingi 508,000,000/- kwa kazi za kawaida na kwa kazi za maendeleo Shillingi 36,500,000/-

## IDARA YA MUFTI WA ZANZIBAR

103. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Idara ya Mufti wa Zanzibar imeendelea vyema katika kutimiza malengo iliyojipangia pamoja na yale yaliopo kwa mujibu wa sheria nambari tisa ya mwaka 2001 inayoipa Idara majukumu mbalimbali ya kiutendaji. Utekelezaji huo ulikuwa kama ifuatavyo:-

104. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia July 2005 hadi March 2006, jumla ya maswali 575 yanayohusu mambo ya kiislamu yaliwasilishwa na wananchi mbalimbali katika Afisi ya Mufti. Kati ya hayo maswali 263 yaliweza kujibiwa ikiwa ni sawa na asilimia 45.7% ya maswali yote yaliyowasilishwa. Aidha jumla ya migogoro 505 ya kifamilia iliyohusisha masuala ya Mirathi, Ndoa, Talaka, na migogoro ya misikiti imetatuliwa kwa kuwapa ushauri wahusika. Aidha migogoro 212 kati ya hiyo ilielekezwa kwa Makadhi wa Wilaya kwa utatuzi zaidi.

105. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Fedha kilichomalizika jumla ya wafanyakazi 7 wamepatiwa fursa ya kujiendeleza kimasomo kwa mchangamano ufuatao: wafanyakazi 2 mwanamke mmoja na mwanamme mmoja wamemaliza masomo ya cheti. Wafanyakazi wawili wanaendelea na mafunzo hayo ya cheti akiwemo mwanamke mmoja na mwanamme mmoja. Kwa upande wa masomo ya muda mrefu wafanyakazi 3 bado wanaendelea na masomo ambapo mwanamke mmoja anachukua Shahada ya kwanza na mwanamme mmoja anachukua Shahada ya Juu (Phd).

106. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Afisi ya Mufti imeweza kutekeleza malengo iliyojipangia kama ifuatavyo:

Kuendeleza mawasiliano na Serikali ya Oman ili kufanikisha ujenzi wa Afisi mpya ya Mufti.

107. Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka jana nilieleza mafanikio ya upatikanaji wa kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Afisi ya Mufti. Naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba juhudi za ujenzi wa Afisi hiyo zinaendelea na tayari makisio ya ujenzi yameshafanywa na kuwasilishwa kwa mfadhili. Kwa hatua za awali makandarasi watatu wamejitokeza kuwania kazi ya ujenzi. Kwa hivi sasa jambo ambalo limechelewesha kazi hii ni kule kubadilika kwa gharama kunakotokana na kupanda kwa bei za vifaa vya ujenzi kunakotafautiana na makisio ya awali. Katika hatua ya kumchagua mkandarasi, Serikali na Mfadhili watashirikiana kwa pamoja.

Kuendeleza juhudi za kuwaelimisha Waumini na wananchi kwa jumla juu ya umuhimu wa amani na utulivu nchini.

108. Mheshimiwa Spika, Afisi ya Mufti wa Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2005 /2006 iliendelea na lengo lake la kuhubiri Amani na Utulivu nchini. Hali hii ilichangiwa zaidi na kuwepo kwa Uchaguzi Mkuu wa Octoba 2005 ambapo kulipelekea suala hili kupewa uzito wa kipekee hasa kwa kuzingatia kwamba asilimia kubwa ya Wazanzibari ni Waislamu.

Pamoja na kuwepo tofauti ndogo ndogo za kiitikadi, bado suala la kuwa na amani na utulivu lina nafasi yake. Katika hilo na kwa kuitumia kamati ya pamoja ya kidini (Inter faith Committee for Peace Builiding) jumla ya Semina sita (6) zilifanyika Unguja na Pemba ambazo zililenga kuwaelimisha Wanasiasa na Wananchi wetu juu ya Amani na Utulivu nchini. Pamoja na wanasiasa Waandishi wa Habari, Vyombo vya Dola, na Vyomba vya Sheria pia vilihudhuria semina hizo.

109. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho pamoja na juhudi hizo, pia Mheshimiwa Mufti wa Zanzibar akifuatana na baadhi ya wasaidizi wake, walifanya ziara rasmi za kutembelea Mikoa yote mitano ya Zanzibar kwa lengo la kuonana na Masheikh na Waumini wa kiislamu pamoja na viongozi mbalimbali wa Serikali na jamii. Ajenda kuu ya ziara hizo ni kuleta utulivu na Amani Visiwani.

Kuendekeza juhudi za kuwaelimisha Maimamu juu ya matumizi ya mwongozo wa kiislamu juu ya UKIMWI

110. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006 Afisi ya Mufti wa Zanzibar imeendeleza juhudi za kuwaelimisha viongozi wa dini ya kiislamu pamoja na waumini wao katika mapambano dhidi ya janga la ukimwi. Katika kipindi hicho taaluma ya kupambana na ukimwi kiislamu ilitolewa kwa maimamu 500 kwa Unguja na Pemba. Hivi sasa Afisi imo mbioni kusimamia namna ya kuunda vikundi vya vijana wapatao ishirini (20) kwa kila msikiti mmoja unaosaliwa sala ya Ijumaa ili kupita nyumba kwa nyumba kutoa taaluma hiyo. Kazi hii imeshaanza kwa baadhi ya misikiti ya Ijumaa kama vile msikiti wa Gongoni, Sebleni, na kadhalika.

111. Mheshimiwa Spika, mbali na malengo hayo iliyojipangia Afisi ya Mufti imeendelea kukuza mashirikiano na Taasisi mbalimbali za ndani na nje katika kipindi cha mwaka 2005/2006. Katika kipindi hicho Afisi ilitembelewa na Mabalozi 2 ambao ni Balozi wa Marekani na Balozi wa Sweden. Pia Idara ya Mufti ilipokea ujumbe wa wahubiri kutoka Afrika ya Kusini, Marekani (The Balm in Gilead), Denmark (DANMISSION) na pia Idara ilipokea Wachunguzi wa Kimataifa wa uchaguzi kutoka kusini mwa Afrika (SADCPF).

112. Mheshimiwa Spika, katika hilo pia Afisi ya Mufti imeweza kushiriki vyema katika wazo la Waislamu wa Afrika Mashariki la kufufua silka na tabia za kiislamu zilizokuwepo zamani (East African Islamic Culture). Vikao viwili vilifanyika kimoja Tanga na kimoja Bagamoyo Tanzania Bara ambapo Afisi ilishiriki. Pamoja na utekelezaji wa malengo hayo kama nilivyoeleza, Afisi ya Mufti ilikabiliwa na matatizo ya uhaba na uchakavu wa vyombo vya usafiri na zana za kufanyia kazi.

113. Mheshimiwa Spika, Afisi ya Mufti wa Zanzibar kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007 imejiwekea malengo yafuatayo:-

i) kuendeleza harakati za upatikanaji wa jengo la Afisi ya Mufti;
ii) kuendelea na jukumu la kutoa Fatwa pamoja na kujibu masuala ya waislamu;
iii) kuendeleza mashirikiano na mashirika ya kiislamu na yasiokua ya kiislamu katika kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kuweka Amani na Utulivu nchini; na
iv) kuendelea na mapambano dhidi ya Ukimwi kwa mtizamo wa Kiislamu.

114. Mheshimiwa Spika, ili Afisi ya Mufti wa Zanzibar iweze kutekeleza malengo ya kazi zake kwa ufanisi zaidi katika mwaka wa fedha 2006/2007 naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 98,601,525/- kwa kazi za kawaida na shilingi 10,350,000 kazi za maendeleo.

## AFISI YA MRAJIS MKUU WA SERIKALI

115. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali nayo imeendelea vizuri katika kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na malengo iliyojipangia kama ifuatavyo:-

### Kufanya mapitio ya Sheria ya Makampuni, Sheria ya Vizazi na Vifo na marekebisho ya "Database" ya usajili wa Makampuni.

116. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuona kwamba Sheria ya Makampuni inarekebishwa na kwa kuzingatia uzito wa kazi hiyo, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali imewasiliana na wafadhili kuisaidia. Katika hilo Benki ya Maendeleo ya Afrika yaani "African Development Bank"(ADB) imekubali kusaidia kupitia "Mpango wa Kusaidia Taasisi katika Kuimarisha Utawala Bora" yaani "Institutional Support Project for Good Governance", ambapo Mapitio ya sheria ya Makampuni ni kipengele kimoja wapo katika mradi wa "Enhancing Good Cooporate Management Practices". Mradi huu umechelewa kuanza kwa sababu ya kuchelewa kutimizwa kwa masharti ya utekelezaji wa mradi wenyewe. Hivi sasa masharti yote yameshatimizwa na tayari Waziri anayesimamia masuala ya Fedha ameshaunda "Steering Committee" itakayosimamia utekelezaji wa mradi.

117. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Nembo za Biashara (Trademark Act) tayari Rasimu mpya ya Nembo za Biashara imeshajadiliwa na Kamati ya Uongozi ya Wizara na hivi sasa inafanyiwa kazi na Afisi kwa kushirikiana na mfadhili wa mradi huu shirika la Umoja

wa Mataifa la “World Intellectual property Organization” (WIPO) ili pamoja na mambo mengine, kuweza kuingiza vipengele vya ulinzi na utunzaji wa “Geographical Indications” na kuzuia “Unfair Competition”

118. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kuifanyia marekebisho “Database” ya usajili wa makampuni utekelezaji wake haukuwa kama ulivyopangwa kutokana na gharama kubwa zinazotakikana. Aidha mawasiliano bado yanaendelea ili kupata ufadhili katika mradi wa "Business Environment Strengthening in Tanzania” ( BEST) ambapo bado wanaonesha hamu ya kutusaidia.

Kukamilisha uwekaji wa mfumo wa kusajili Vizazi na Vifo kwa kutumia kompyuta yaani “Computerization of Birth and Death Registration System”

119. Mheshimiwa Spika, kazi hii imeendelea kutekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha ambapo Shirika la Maendeleo la Kimataifa (UNDP) limekubali kutoa Kompyuta 16 hadi sasa kompyuta 6 zimeshatolewa kwa kazi hiyo, kompyuta 10 zilizobakia zitakabidhiwa katika Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali katika mwaka wa fedha wa 2006/2007.

120. Mheshimiwa Spika, vilevile utekelezaji wa lengo hili umechelewa kufuatia haja ya kuwa na marekebisho ya sheria ya vizazi na vifo, sheria ambayo ndio inayotoa maelekezo ya kiutendaji. Kazi ya kuifanyia marekebisho sheria hayo imeanza katika ngazi za awali kwa kutoa mapendekezo ambayo hatimae yatajadiliwa na Baraza lako tukufu.

Kujenga uwezo wa Afisi za uandikishaji wa Vizazi na Vifo za Wilaya ili ziweze kwenda sambamba na matakwa ya mfumo mpya.

121. Mheshimiwa Spika, katika kujitayarisha na mfumo mpya wa usajili, Idara ya Mrajis Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Afisi Kuu Pemba imeweza kutoa mafunzo ya Kompyuta kwa Maafisa wake wa Wilaya. Kwa kuanzia maafisa wa Wilaya nne za Pemba na mbili za Unguja wameshapata mafunzo hayo. Mafunzo hayo yataendelea kwa maafisa wa wilaya nyengine hadi wilaya zote zitakapomalizika.

122. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa jengo la Pemba la Usajili ambalo limekuwa likilalamikiwa kutokana na ufinyu wake wa nafasi, ujenzi wa jengo jipya umefikia hatua za mwisho na unatarajiwa kukamilika wakati wowote mara fedha za kumalizia kazi hiyo zitakapopatikana. Utakapokamilika ujenzi huo, Afisi itakuwa na nafasi ya kutosha ya kuweza kuhimili ongezeko la wafanyakazi na kazi zenyewe.

Kukamilisha mapitio ya sheria ya Vizazi na Vifo.

123. Mheshimiwa Spika, kama maelezo ya awali yalivyojieleza kuhusu mfumo wa kusajili vizazi na vifo kwa kutumia kompyuta, mfumo huo unaenda sambamba na urekebishaji wa sheria husika.

124. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006 kazi ya mapitio ya sheria ya vizazi na vifo iliendelea kwa mshauri "Consultant" kukamilisha kazi ya kutoa mapendekezo juu ya marekebisho ya sheria hiyo ya vizazi na vifo na baadae kupitiwa na jopo la wataalam mbalimbali, rasimu ya mswada wa sheria mpya ya Vizazi na Vifo uliwasilishwa Wizarani na kujadiliwa na Kamati ya Uongozi ya Wizara.

Mafunzo kwa Wafanyakazi.

125. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006 jumla ya wafanyakazi 8 wamepatiwa mafunzo kati ya hao 2 wamehudhuria masomo ya muda mfupi na wafanyakazi 6 wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu. Kati ya hao wanaume 5 na wanawake ni 3. Aidha jumla ya wafanyakazi sita wanaendelea na mafunzo yao katika vyuo mbalimbali kati yao wanawake ni watatu na wanaume watatu. Jumla ya wafanyakazi wanne wamehitimu mafunzo ya sheria katika kiwango cha cheti katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na mfanyakazi mmoja amemaliza katika kiwango cha stashahada ya juu ya Teknolojia ya habari (Information Technology) katika chuo cha Usimamizi wa Fedha, na mwengine katika kiwango cha "degree" ya kwanza ya sheria katika Chuo Kikuu cha Zanzibar.

126. Mheshimiwa Spika, katika kufikia lengo lililokusudiwa la kuwa na takwimu sahihi za usajili na utunzaji mzuri wa kumbukumbu, Afisi ya Mrajis Mkuu imewapatia wafanyakazi wake wawili mafunzo ya wiki nane ya "Documentation and Records Management". Mafunzo hayo yalifanyika katika chuo cha "School of Library, Archives and Documentation Studies" huko Bagamoyo, yamefadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la (UNDP).

Kuzifanyia marekebisho fomu za kukusanyia taarifa za B1 na D1

127. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006 fomu za BI na DI zimefanyiwa marekebisho. Lengo la marekebisho hayo ni kuziwezesha fomu hizo zikusanye taarifa nyingi zaidi ya ilivyo sasa. Aidha imekusudiwa kwamba na fomu nyengine zitafuata utaratibu huo huo kadiri marekebisho ya sheria husika yatakavyofanywa na pia kwa kutegemea hali ya fedha ilivyo.

Kazi za Usajili

128. Mheshimiwa Spika, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali katika kipindi hiki cha 2005/2006 imesajili nyaraka za aina mbalimbali kama ifuatavyo: Kwa mwaka huu wa fedha hadi March Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali iliweza kusajili Jumla ya Vizazi 19,568 na Vifo 1,500. *Kama kiambatisho Na …… kinavyoonesha.*

129. Mheshimiwa Spika, jumla ya tirka za Mali maiti 29 zilishughulikiwa kwa wasiokuwa Waislam kati yao waliokwenda kufungua faili kwa kurithishwa ni 15, waliorithishwa ni 10 waliokuwa bado hawajarithishwa ni 5.

130. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Usajili Makampuni Afisi imeweza kusajili jumla ya Kampuni 80 hadi kufikia mwezi wa Machi 2006. Aidha katika kipindi hicho Majina ya Biashara 86 yamesajiliwa, 43 yakiwa ni ya mtu mmoja mmoja na 21 ni ya ubia. Aidha alama za biashara zilizosajiliwa hadi hivi sasa ni 150. Kwa upande wa alama za uvumbuzi, ni alama moja tu hadi sasa iliyosajiliwa.

131. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ndoa kwa kipindi chote hiki Afisi ilikuwa imekabiliwa na tatizo la ukosefu wa mabuku ya usajili wa ndoa, na ni hivi karibuni tu; kuanzia mwanzoni mwa mwezi wa Febuari 2006 Afisi imeweza kupata mabuku 100 ya ndoa kati ya mabuku 2000 yolioagizwa na kulipia kutoka kwa Mchapishaji Mkuu wa Serikali. Kwa upande wa nyaraka, jumla ya Nyaraka zilizosajiliwa ni 512. Aina za nyaraka hizo ni kama zinavyoonekana hapo chini.

132. Mheshimiwa Spika, katika jukumu la usajili na ufuatiliaji wa jumuiya zisizo za kiserikali (NGO) Jumla ya jumuiya 29 zimesajiliwa. Jumuiya 17 zinasubiri kusajiliwa na kuna maombi 5 mapya yaliyopokelewa.

133. Mheshimiwa Spika, kwa ujumla suala au dhana nzima ya miliki bunifu imekuwa ni ngeni katika jamii yetu ya kizanzibari, hata hivyo tatizo hili si kwa Zanzibar peke yake bali lipo katika nchi nyingi wanachama wa ARIPO “African Region Intellectual Property Organisation”. Katika kutatua tatizo hilo nchi wanachama wa ARIPO pamoja na mambo mengine, katika kikao chake cha Mawaziri kilichofanyika nchini Uganda mwishoni mwa mwaka jana kilidhamiria kila nchi mwanachama kuunda “IP TEAM” ambayo itakuwa na lengo la kuendeleza na kuikuza dhana nzima ya milki ubunifu katika nchi husika.

134. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza hilo Zanzibar, kupitia Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali, tayari imeshateuwa majina ya wajumbe

watakaounda timu hiyo na tayari majina hayo yameshatumwa katika afisi za WIPO kama ilivyokubalika. Katika kuhakikisha hiyo timu inakuwa na uwelewa kuhusiana na dhana ya IP, Afisi ya Mrajis iko katika harakati za kuwasiliana na WIPO ili kuweza kuandaa semina ya wajumbe wote wanaounda timu hiyo.

135. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2005/2006 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 120,000,000/- Kuanzia mwezi Julai 2005 hadi Machi 2006 Afisi imekusanya shillingi 71,264,005/- Idadi hiyo ya fedha zilizokusanywa ni sawa na asilimia 59.4 ya malengo iliyojiwekea. Aidha kwa mwaka mpya wa fedha 2006/2007, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali inakusudia kukusanya na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali jumla ya shilingi 124,113,000/-

136. Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada zilizochukuliwa na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu yake, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali bado inakabiliwa na matatizo mengi, likiwemo la uchakavu wa jengo la Afisi, uhaba wa vitendea kazi na vyombo vya usafiri.

137. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali inakabiliana na ongezeko la kazi, kuondoa kero kwa wananchi na kuongeza ufanisi kazini kama ni chachu muhimu kwa mafanikio bora ya Afisi hii, hivyo katika kipindi cha mwaka 2006/2007 inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:

i) kuharakisha ukamilishaji wa utengenezaji wa mfumo mpya wa usajili wa vizazi na vifo;
ii) kukamilisha marekebisho ya Sheria mpya ya vizazi na vifo;
iii) kufanya semina kwa watendaji wa Wilaya kuhusu usajili wa vizazi na vifo kwa kutumia kompyuta;
iv) kuwapatia mafunzo watendaji wake katika taaluma mbalimbali ikiwemo “database management”;
v) kuanza kufanya marekebisho ya Sheria ya makampuni;
vi) kuunda IP TEAM na kuhakikisha inafanya kazi zake; na
vii) kununua zana za kutendea kazi.

138. Mheshimiwa Spika, ili Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali iweze kutekeleza malengo yake iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2006/2007 naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 148,293,975/- kwa matumizi ya kawaida.

AFISI YA MSAJILI WA HAKIMILIKI

139. Mheshimiwa Spika, Afisi hii ni mpya na imeundwa kwa mujibu wa sheria ya Hakimiliki namba 14 ya mwaka 2003. Kuanzishwa kwa Afisi hii kumelengwa kusimamia moja kwa moja maslahi ya wasanii na watengenezaji wa kazi za sanaa wa Zanzibar na wa nje ya Zanzibar. Aidha kwa upande mwengine ni kwenda sambamba na kutekeleza mikataba ya kimataifa kuhusiana na suala zima la Hakimiliki.

140. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa shughuli za Afisi katika mwaka wa fedha 2005/2006 uilikuwa ni mgumu na wenye matatizo kutokana na afisi hii kutokuwa na bajeti yake kulikotokana na kuanza kazi katikati ya mwaka wa fedha. Hali hiyo ilipelekea Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali na Wizara kutoa msaada. Vilevile Afisi inapokea misaada na ushirikiano mkubwa kutoka Shirika la Kiulimwengu la Kimataifa linaloshugulikia milki bunifu (World Intellectual Property Organization - WIPO), Shirika la Ulimwengu lisilo la kiserikali la watunzi (International Confederation of Society of Authors and Composers - CISAC) pamoja na kutoka afisi za jumuiya dada za kikanda za COSOTA(Copyright Society of Tanzania) na COSOMA (Copyright Society of Malawi) . Aidha kukosekana kwa watendaji wengine kulipelekea ugumu wa utendaji na pia uchelewaji wa kuanza kutekeleza malengo ya jumuiya kama yalivyopangwa. Hata hivyo Afisi iliweza kutekeleza baadhi ya mambo ya msingi,ikiwa ni pamoja na :-

i) kuhudhuria kwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Hakimiliki katika mafunzo ya vitendo Tanzania bara kwa kipindi cha wiki moja;
ii) kutoa elimu kwa njia ya redio;
iii) kutafsiri sheria ya Hakimiliki na kuandaa rasimu za kanuni za utoaji leseni

141. Mheshimiwa Spika, Afisi hii kwa mwaka huu wa fedha 2006/2007 imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo;

i) kuwapatia mafunzo ya hakimiliki watendaji watakao ajiriwa, wajumbe wa Bodi ya hakimiliki, wasanii, watengenezaji wa kazi za sanaa, watumiaji wa kazi za sanaa, pamoja na wanafunzi katika skuli ya muziki iliyopo Zanzibar “THE DHOW SCHOOL OF MUSIC”;
ii) kuelimisha jamii kwa njia ya redio na televisheni juu ya masuala ya Hakimiliki;
iii) kuanzisha harakati za kujiunga na jumuiya za kikanda na za kimataifa zenye malengo yanayofanana;
iv) kuandaa utaratibu wa usajili na utunzaji wa kazi za sanaa, vyama vya watunzi, wasanii, watayarishaji wa kanda za sauti zilizorikodiwa, watangazaji na wachapishaji;

v) kuandaa utaratitibu wa kupokea na kuthibitisha maombi ya kufanya shughuli za sanaa Zanzibar, kwa wasanii wa ndani na nje ya Zanzibar. Hii ni kwa mashirikiano ya pamoja na Baraza la Sanaa (BASAZA), Bodi ya Sensa Zanzibar, Mamlaka ya Mapato na Idara ya Uhamiaji; na
vi) kuandaa utaratibu wa kutoa leseni kwa watumiaji wa kazi za sanaa ili kuruhusu matumizi halali ya kazi hizo.

142. Mheshimiwa Spika, ili Afisi hii iweze kutekeleza malengo iliyojiwekea naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha ruzuku ya shilingi 118,000,000/- kwa kazi za kawaida.

KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA

143. Mheshimiwa Spika, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ni miongoni mwa Taasisi zilizomo katika Wizara yangu. Taasisi hii ina jukumu la kusimamia mali zilizowekwa Wakfu, mirathi ya Waislamu, kuongoza shughuli za Hijja, Sala na Mabaraza ya Iddi, misaada ya Kiislamu na mambo mengine ya kidini inayopangiwa.Kamisheni imeendelea kutekeleza malengo iliyojipangia kwa kiwango cha kuridhisha kama ifuatavyo:

Kuendelea na ufuatiliaji wa madeni sugu ya Taasisi za Serikali.
144. Mheshimiwa Spika, Kamisheni iliendelea kufuatilia madeni yake sugu kwa Taasisi za Serikali. Kwa upande wa Taasisi za Serikali kati ya shilingi 26,005,000/- zinazodaiwa jumla ya shilingi 2,000,000/- tu, sawa na asilimia 7.69% ya deni hilo ndio zimelipwa katika kipindi cha hadi kufikia Machi 2006. Kwa sasa deni lililobakia ni shilingi 11,005,000/- kwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, na shilingi 13,000,000/- kwa Wizara ya Fedha na Uchumi. Jumla ni shilingi 24,005,000/-. Kwa upande wa wateja binafsi jumla ya shilingi ……. zimekusanywa sawa na asilimia ……. ya deni lote la shilingi ……. inazowadai wateja wa kibinafsi.

145. Mheshimiwa Spika, Kamisheni imekuwa ikitumia njia mbalimbali katika ufuatiliaji wa madeni yake ikiwa ni pamoja na kuwafuatilia wateja wake nyumba hadi nyumba, kufanya vikao na majadiliano na wenye madeni na kuwapelekea na kwa kuwakumbusha kupitia barua . Aidha Kamati maalum ya wajumbe wa Bodi ya Kamisheni wamekuwa wakifuatilia madeni ya Taasisi za Serikali katika siku zote wanazopewa miadi na taasisi hizo.

Kukamilisha kazi ya marekebisho ya Sheria namba 5 ya mwaka 1980, ili iweze kuwa mwongozo wa utendaji mzuri wa Kamisheni.

146. Mheshimiwa Spika, kazi ya marekebisho ya Sheria Namb.5 ya mwaka 1980, ili iweze kuwa mwongozo wa utendaji mzuri wa Kamisheni katika zama hizi za utawala bora imo katika hatua za mwisho kukamilika ili ipitishwe katika utaratibu hadi kuletwa katika Baraza La Wawakilishi. Wizara iliteua wanasheria wazoefu wa majukumu na utendaji wa kila siku wa Kamisheni ili waisimamie kazi hiyo. Kukamilika kwa sheria hiyo kutaisaidia Kamisheni katika usimamizi wa mirathi na mali za Wakfu na kuwabana wapangaji wasiolipa ipasavyo. Wataalamu wamo katika hatua za mwisho za kukamilisha mapitio ya sheria na kuanza kuitumia.

147. Mheshimiwa Spika, katika utendaji wake wa kila siku na utoaji huduma, Kamisheni ya Wakfu kupitia vitengo vyake sita imeendelea na shughuli zake ilizopangiwa kama ifuatavyo:-

Kitengo cha Urithi

148. Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Urithi hushughulikia masuala yote ya mirathi ya Waislamu ambayo hufikishwa Kamisheni. Aidha hutoa taaluma na ushauri wa kisharia kuhusiana na mas-ala ya mirathi, husuluhisha mizozo ya migogoro inayosababishwa na mirathi na kuweka kumbukumbu muhimu kuhusiana na nyaraka za mirathi.

149. Mheshimiwa Spika, Kamisheni imeanzisha utaratibu wa kuhifadhi kumbukumbu za mirathi katika kompyuta katika kipindi cha Julai 2005 hadi Machi 2006 kitengo cha urithi kimefungua tirka mpya 478, tirka zilizofungwa ni 191 ambazo zina mali yenye thamani ya shilingi 23,225,636.50 na tirka 287 bado zinaendelea kushughulikiwa.

150. Mheshimiwa Spika, kitengo cha urithi kinapokea wananchi wengi ambao hutaka ufafanuzi na miongozo kuhusiana na mambo ya mirathi na kutoa taaluma hiyo kupitia vyombo vya habari na kupitia majukwaa mbalimbali kila inapohitajika.

151. Mheshimiwa Spika, kitengo cha urithi kwa sasa kinatunza fedha za mayatima 241 hadi wafikie umri wa kutaswarafu mambo yao kwa mashirikiano na wadhamini wao. Aidha kitengo kimeweza kusuluhisha jumla ya mizozo 172, usuluhishi wa mizozo 41 unaendela na mizozo 21 imepelekwa Mahakamani ili kupatiwa ufumbuzi.

152. Mheshimiwa Spika, kwa vile Kamisheni ya Wakf na Mali ya Amana ni taasisi yenye hadhi ya kushitaki, kushtakiwa na kushirikishwa katika kesi za Wakfu, Mirathi na shughuli za Kiislamu, katika kipindi Julai 2005

hadi Machi 2006 imeshughulikia jumla ya kesi 30 Mahakamani. Kati ya kesi hizo, mbili (moja ya urithi na moja ya Wakfu) zilifunguliwa na Kamisheni na kesi 28 (21 za mirathi, 5 za Wakfu na 2 za Shughuli za Kiislamu) zilifunguliwa dhidi ya Kamisheni ikiwa ni kati ya wadaiwa. Kati ya kesi hizo, 13 zimeshatolewa hukumu na kesi 15 zinaendelea.

## Kitengo cha Wakfu na Amana

153. Mheshimiwa Spika, kitengo cha Wakfu na Amana ni muhimu sana ambacho hushughulikia mali za watu ambazo zimewekwa Wakfu kwa shughuli za dini, mambo ya kheri na hata familia. Pia huhifadhi na kusimamia mali za Amana zikiwemo za mayatima, taasisi n.k.

154. Mheshimiwa Spika, hivi sasa Kamisheni inasimamia nyumba 451, kati ya hizo nyumba 385 ni za Wakfu na nyumba 66 ni za Amana. Jumla ya nyumba nne za Amana zimerejeshwa kwa wenyewe katika kipindi cha mwaka uliopita baada ya wenyewe kufikia umri wa kutaswarafu mambo yao na kukamilisha taratibu maalum zilizopo za kuomba. Aidha kitengo kinasimamia jumla ya vikataa 12 vya Wakfu.

155. Mheshimiwa Spika, jumla ya fedha zilizokusanywa kwa kipindi cha Julai 2005 hadi Machi 2006 ni shilingi 59,099,900/- kati ya 67,000,000/- ilizokusudia kukusanya. Hii ni sawa na asilimia 88.21% ya lengo. Aidha Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana imezifanyia matengenezo jumla ya nyumba 14 za Wakfu na kuyasafisha mashamba. Kazi hizi zimegharimu jumla ya shilingi 23,651,000/-.

156. Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa bado suala la wadaiwa linaisumbua sana Kamisheni. Madeni hayo ya Taasisi za Serikali na watu binafsi hadi kufikia Machi 2006 yalikuwa ni jumla ya shilingi 107,605,942/-. Tunatarajia sheria mpya ya Kamisheni itatoa mamlaka ya kuwachukulia hatua kali wale wadaiwa wote walio wakorofi.

157. Mheshimiwa Spika, katika kuleta ufanisi wa uhifadhi wa Mali za Wakfu na Amana Kamisheni ya Wakfu imeanza kuhifadhi katika kompyuta kumbukumbu zote muhimu zinazohusu mali hizo. Kamisheni inaishukuru Asasi ya Aga Khan kwa kusaidia kazi hiyo.

## Kitengo cha Shughuli za Kiislamu na Uhusiano

158. Mheshimiwa Spika, kitengo cha shughuli za kiislamu na kile cha uhusiano viliandaa sala na mabaraza ya Idd el Fitri na Idd el Hajj. Pia imefanikisha kupatikana msaada wa kulipiwa gharama za masomo ya Uimamu ya miaka mitatu nchini Algeria. Jumla ya vijana wanne (wawili kutoka Unguja na wawili kutoka Pemba) wamehudhuria masomo hayo.

159. Mheshimiwa Spika, Kamisheni imesimamia ugawaji wa sadaka na nyama ya kondoo inayotolewa na "Islamic Development Bank", pia imekuwa ikishirikiana kwa karibu kabisa na mashirika na taasisi za nje na ndani katika kufanikisha upatikanaji na ugawaji wa misaada mbalimbali kutoka nje na ndani. Kamisheni inatoa shukrani za dhati kwa mashirika ya Africa Muslims Agency, Al – Yusouf Charitable Society, Al-Noor Charitable Society for the Needy, African Charitable Society, Jumuia ya Istiqama, Wakfu wa Mazrui na nyenginezo kwa misaada yao mingi kwa jamii yetu.

160. Mheshimiwa Spika, Kamisheni ya Wakfu kwa kushirikiana na vikundi vinavyoshughulikia safari za Hijja ilifanikisha safari ya Mahujaji 653 waliokwenda Hijja mwaka huu kwa kupitia vikundi vya Zanzibar. Majina ya vikundi, idadi ya jumla ya Mahujaji kwa kila kikundi, idadi ya Mahujaji waliotokea Zanzibar na gharama za safari kwa kila kikundi zimebainishwa katika *kiambatisho Na. 14*. Aidha katika Hijja iliyopita Kamisheni ilikuwa ndie mdhamini wa Mahujaji wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kitengo cha Utawala na Utumishi

161. Mheshimiwa Spika, kitengo cha Utawala na Utumishi ni kitengo muhimu katika kuhakikisha kuwa shughuli za kila siku za utendaji ndani ya Kamisheni zinafanyika kwa ufanisi mkubwa. Aidha kinasimamia haki na wajibu, nidhamu za wafanyakazi, maslahi yao, upatikanaji na utunzaji wa vitendea kazi na kusimamia mazingira ya ujumla ya ofisi za Kamisheni.

162. Mheshimiwa Spika, ili kuendana na mahitaji ya karne tuliyonayo ya sayansi na teknolojia, suala la taaluma na mawasiliano limepewa kipaumbele katika Kamisheni. Jumla ya wafanyakazi watatu wameanza masomo mwaka huu, ambapo mwanamme mmoja anasomea cheti cha sheria katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na wawili, (mwanamme na mwanamke) wapo Chuo cha Utumishi Serikalini. Aidha Wafanyakazi wanne( wanawake wawili na wanaume wawili) wanaendelea na masomo, mmoja shahada ya uzamili ya utawala nchini Uganda, mmoja shahada ya kwanza ya sheria (LLB) nchini Urusi na wawili stashahada ya Uhasibu katika Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka.

163. Mheshimiwa Spika, pamoja na mafaniko yaliyopatikana Kamisheni ya Wakfu inakabiliwa na matatizo yafuatayo:

i) ufinyu wa nafasi katika ofisi zake na imekuwa inaomba kurejeshewa sehemu ya jengo lake ambayo kwa sasa inatumika kama ni Mahkama ya Kazi (Industrial Court),
ii) upungufu wa vitendea kazi hasa kompyuta,

iii) kuchelewa kutolewa hukumu kwa kesi zilizopo Mahakamani jambo ambalo huchelewesha kutoa haki za watu,
iv) ukorofi wa baadhi ya watu katika kulipa kodi na wengine kukodisha kwa bei kubwa kabisa bila ya idhini ya Kamisheni.

164. Mheshimiwa Spika, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana imejiwekea kutekeleza malengo yafuatayo kwa mwaka wa 2006/2007 :-
i) kukamilisha matayarisho ya Sheria na kuanza kuitumia;
ii) kuendeleza kazi ya kuhifadhi kumbukumbu zote za nyakfu, Amana na Mirathi;
iii) kuwaendeleza wafanyakazi wake kitaaluma; na
iv) kupunguza tatizo la vitendea kazi hasa kompyuta na samani.

165. Mheshimiwa Spika, ili Kamisheni ya Wakfu iweze kumudu na kutekeleza vyema mipango na majukumu yake katika kipindi cha 2006/2007 naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe ruzuku ya shilingi 130,661,559/-

AFISI KUU PEMBA

166. Mheshimiwa Spika, Afisi Kuu Pemba ni kiungo muhimu cha Wizara Makao Makuu Zanzibar na Idara na Taasisi kwa upande wa Pemba katika kuratibu na kusimamia shughuli za mipango ya Wizara. Afisi Kuu imeendelea na kutekeleza majukumu yake kwa kiwango kikubwa mbali na matatizo ya Fedha na wafanyakazi wenye taaluma ya juu hasa katika masuala ya Utawala Bora, ambapo inahitajika katika kuwaondoshea kero wananchi na kuwaletea maendeleo endelevu. Ni matumaini ya Afisi kwamba itatekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa katika mwaka ujao wa Fedha 2006/2007, ili kukidhi mustakbali wa Utawala bora na mkakati wa kupunguza umaskini Zanzibar. katika kipindi cha mwaka 2005/2006 Afisi Kuu Pemba imeendelea kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo.

Kuwaendeleza wafanyakazi kitaaluma
167. Mheshimiwa Spika, katika hatua ya kuwaendeleza wafanyakazi kitaaluma Afisi kuu imekuwa mstari wa mbele kuhakikisha wafanyakazi wanapatiwa taaluma. Jumla ya wafanyakazi watatu wako masomoni, wawili Chuo Kikuu Tunguu na mmoja Cheti, kati ya wafanyakazi hao mmoja ni mwanamke na wawili wanaume.

168. Mheshimiwa Spika, mbali ya utekelezaji wa majukumu yake iliyojipangia Afisi pia imetoa mafunzo ya Semina ya kuelimisha wafanyakazi juu ya janga hatari la Ukimwi ili waweze kuelewa athari za

Ukimwi na njia za kujikinga. Jumla ya wafanyakazi 100 kutoka Idara zote za Wizara Pemba walishiriki katika mafunzo hayo.

169. Mheshimiwa Spika, aidha Afisi Kuu – Pemba kupitia kitengo cha NGO's imeendelea kuratibu jumuiya zisizo za Kiserikali na kuzipatia maelekezo na mbinu za kiutendaji ili ziweze kutekeleza vizuri malengo ya jumuiya zao kwa lengo la kuleta maendeleo endelevu kwa jamii husika na Taifa kwa ujumla.

170. Mheshimiwa Spika, jumla ya shilingi 90,483,821/- zimeingizwa hadi kufikia Machi 2006 ambapo shilingi 80,345,907/- sawa na asilimia 88.8% zimetumika kwa kulipia mishahara na shilingi 10,138,712/- sawa na asilimia 11.2% zimetumika kwa matumizi mengineyo.

171. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/2007 pamoja na majukumu ya kuratibu shughuli za Wizara Afisi Kuu – Pemba inakusudia kuendelea kutekeleza malengo yafuatayo:

i) kufanya matengenezo ya nyumba ya Wizara;
ii) kuwaendeleza wafanyakazi kitaaluma katika mafunzo ya muda mrefu na mfupi;
iii) kuendelea kutafuta fedha za kununua vifaa na nyenzo muhimu za kazi ikiwemo vipando; na
iv) kuendelea na mpango wa kutoa elimu ya ukimwi kwa wafanyakazi.

172. Mheshimiwa Spika, ili Afisi Kuu Pemba iweze kutekeleza malengo iliyojipangia katika mwaka wa fedha 2006/2007 inaomba kuindhinishiwa jumla ya shilingi 231,930,000/-

## SHUKURANI

173. Mheshimiwa Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuiwasilisha Hotuba hii mbele ya Baraza lako tukufu. Aidha haitokuwa jambo la busara kama sitatoa shukurani zangu za dhati kwa wale wote waliotoa michango yao katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara pamoja na Taasisi zake zote. Shukurani maalum nazitoa kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako tukufu. Sambamba na hilo natoa shukurani kwa watendaji wakuu wa taasisi za Wizara yangu kwa hatua nzuri ya kiutendaji iliyofikiwa hasa ukizingatia uchanga na majukumu makubwa ya Wizara yangu. Vilevile kwa niaba ya watendaji wa Wizara yangu napenda kutoa shukurani kwa wajumbe wa Baraza hili kwa michango yao mizuri na yenye manufaa kwa Wizara na Taifa kwa ujumla.

174. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa ikifanya kazi zake kwa mashirikiano na wafadhili na wahisani mbalimbali na kwa heshima na taadhima naomba ruhusa yako kuwashukuru wale wote wanaotusaidia. Nao ni UNDP, ADB, WIPO, GLOBAL FUND na WORLD BANK, Africa Muslims Agency, Al - Yousaif Charitable Society, Serikali ya Oman, Serikali ya Saud Arabia, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tume ya UKIMWI ya Zanzibar (ZAC) na Vikundi mbalimbali vilivyosafirisha Mahujaji.

HITIMISHO

175. Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naomba wajumbe wa Baraza lako tukufu waidhinishe matumizi ya wizara yangu kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007 jumla ya shilingi 3,145,401,730/- kwa kazi za kawaida na shilingi 276,618,000/- kwa kazi za maendeleo ili iweze kutekeleza malengo yake iliyojipangia. Aidha naliomba Baraza lako likubali mchango wa shilingi 152,613,000/- ikiwa ni mapato yatakayokusanywa na wizara hii ambayo yataingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. *Viambatisho Na. 2 na Na. 4 vinahusika*.

176. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

RAMADHAN ABDALLA SHAABANI
WAZIRI WA NCHI (AR)
KATIBA NA UTAWALA BORA
ZANZIBAR.

KIAMBATISHO NAMBA 1: FEDHA ZILIZOINGIZWA KWA MALIPO YA MISHAHARA NA MATUMIZI MENGINEYO 2005/2006

| FUNGU | IDARA | FEDHA ZILIZOIDHINISHWA 2005/2006 | JUMLA FEDHA ZILIZOINGIZWA JULY - MARCH 2005/2006 | WASTANI WA JUMLA (%) | FEDHA ZILIZOINGIZWA JULAI 2005 - MAR - 2006 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | MSHAHARA NA MAPOSHO | (%) | MATUMIZI MENGINEYO | (%) |
| 11 | Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali | 486,579,000.00 | 262,361,661.65 | 54.00% | 235,551,246.00 | 89.78% | 26,810,415.65 | 10.22% |
| 14 | Mahkama | 775,035,000.00 | 526,393,414.00 | 67.92% | 453,022,767.00 | 86.06% | 73,370,647.00 | 13.94% |
| 15 | Afisi ya Mwanasheria Mkuu | 240,072,000.00 | 157,089,632.00 | 65% | 120,303,973.00 | 76.58% | 36,785,659.00 | 23.42% |
| 33/03 | Afisi Kuu Pemba -KUB | 251,292,000.00 | 90,484,619.80 | 36% | 80,345,907.00 | 88.80% | 10,138,712.80 | 11.20% |
| 33/04 | Utawala na Uendeshaji | 378,370,000.00 | 136,480,589.00 | 36% | 85,364,169.00 | 62.55% | 51,116,420.00 | 37.45% |
| 33/05 | Afisi ya Mufti wa Zanzibar | 82,226,000.00 | 66,042,341.00 | 80.32% | 39,780,841.00 | 60.20% | 26,311,500.00 | 39.80% |
| 33/07 | Idara ya Kuratibu shughuli za Utawala Bora | 29,122,000.00 | 4,723,367.00 | 16.22% | 2,966,217.00 | 62.80% | 1,757,150.00 | 37.20% |
| 33/09 | Mamlaka ya Kuzuia na Kusimamia Maadili ya Viongozi | 68,806,000.00 | 5,354,720.00 | 7.78% | 3,597,570.00 | 67.20% | 1,757,150.00 | 32.80% |
| 33/11 | Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali | 113,002,000.00 | 114,600,048.00 | 101.41% | 63,999,374.00 | 55.85% | 50,600,674.00 | 44.15% |
| 35 | Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka | 208,259,000.00 | 112,865,090.00 | 54.19% | 77,837,436.00 | 69.00% | 35,027,654.00 | 31.00% |
| Kasma | Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana | 79,646,000.00 | 79,422,091.00 | 99.72% | 79,422,091.00 | 99.72% | - | - |
| 33/12 | Afisi ya Mrajis Mkuu Pemba | 25,083,000.00 | 15,078,814.00 | 60.12% | 12,862,314.00 | 85.30% | 2,216,500.00 | 14.70% |
| Kasma | Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Pemba | 34,682,000.00 | 24,892,000.00 | 71.78 | 24,892,000.00 | 71.78% | - | - |
| | JUMLA | 2,772,174,000.00 | 1,595,788,387.45 | 57.6 | 1,279,945,905.00 | 80.21% | 315,892,482.45 | 19.79% |

KIAMBATISHO NAMBA 2: MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA KAZI ZA KAWAIDA NA MAENDELEO 2006/2007

| FUNGU | IDARA | KAZI ZA KAWAIDA | | | KAZI ZA MAENDELEO | JUMLA KUU |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | UNGUJA | PEMBA | JUMLA | | |
| 11 | Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali | 401,295,575.00 | 106,704,425.00 | 508,000,000.00 | 11,418,000.00 | 519,418,000.00 |
| 14 | Mahakama Kuu | 608,667,000.00 | 240,333,000.00 | 849,000,000.00 | - | 849,000,000.00 |
| 15 | Afisi ya Mwanasheria Mkuu | 336,563,000.00 | - | 336,563,000.00 | - | 336,563,000.00 |
| 33/03 | Afisi Kuu Pemba - (KUB) | - | 231,930,000.00 | 231,930,000.00 | - | 231,930,000.00 |
| 33/04 | Utawala na Uendeshaji | 291,507,000.00 | - | 291,507,000.00 | 19,650,000.00 | 311,157,000.00 |
| 33/05 | Afisi ya Mufti wa Zanzibar | 98,601,000.00 | - | 98,601,000.00 | 10,350,000.00 | 108,951,000.00 |
| 33/07 | Kuratibu Shughuli za Utawala Bora | 29,917,000.00 | - | 29,917,000.00 | - | 29,917,000.00 |
| 33/09 | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kusimamia Maadili ya Viongozi | 54,092,000.00 | - | 54,092,000.00 | - | 54,092,000.00 |
| 33/11 | Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali | 123,939,000.00 | 24,353,000.00 | 148,292,000.00 | - | 148,292,000.00 |
| 35 | Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka | 271,693,000.00 | 99,307,000.00 | 371,000,000.00 | 196,000,000.00 | 567,000,000.00 |
| KASMA | Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana | 85,340,000.00 | 40,121,000.00 | 125,461,000.00 | - | 125,461,000.00 |
| KASMA | Hakimiliki | 118,000,000.00 | - | 118,000,000.00 | | 118,000,000.00 |
| | JUMLA | 2,419,614,575.00 | 742,748,425.00 | 3,162,363,000.00 | 237,418,000.00 | 3,399,781,000.00 |

KIAMBATISHO NAMBA 3: MAKUSANYO YA MAPATO KWA MWAKA 2006/2007

| KIFUNGU | IDARA | FEDHAZILIZOIDHINISHWA 2005/2006 | FEDHA ZILIZOKUSANYWA JULAI 05 – MACHI 06 | ASILIMIA % |
|---|---|---|---|---|
| 11 | Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu SMZ | 2,500,000 | 1,890,000 | 75.6% |
| 14 | Mahkama | 32,500,000 | 10,554,585 | 32.5% |
| 33/11 | Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali | 120,000,000 | 71,264,005 | 59.39% |
| | JUMLA | 155,000,000 | 83,708,590 | 54% |

KIAMBATISHO NAMBA 4: MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA 2006/2007

| FUNGU | IDARA | FEDHA ZILIZOIDHINISHWA MWAKA 2005/2006 | MAKADIRIO KWA MWAKA 2006/2007 | PUNGUFU /ZIADA |
|---|---|---|---|---|
| 11 | Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu | 2,500,000 | 3,000,000 | 500,000 |
| 14 | Mahkama | 32,500,000 | 25,500,000 | (7,000,000) |
| 33/11 | Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali | 120,000,000 | 124,113,000 | 4,113,000 |
| | JUMLA | 155,000,000 | 152,613,000 | -2,387,000 |

KIAMBATISHO NAMBA 5 : FEDHA ZILIZOINGIZWA KWA KAZI ZA MAENDELEO 2005/2006

| FUNGU | AINA YA MRADI | FEDHA ZILIZOIDHINISHWA 2005/2006 | | | FEDHA ZILIZOINGIZWA JULAI 05 - MACHI 06 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MCHANGO WA SERIKALI | MCHANGO WA WAHISANI | JUMLA | MCHANGO WA SERIKALI | MCHANGO WA WAHISANI | JUMLA |
| 72200 | Mradi wa Kuimarisha Utawala Bora | 18,650,000 | 20,400,000.00 | 39,050,000.00 | - | 13,976,400.00 | 13,976,400.00 |
| 72210 | Mradi wa Kuimarisha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali | 19,000,000.00 | 19,859,750.00 | 38,859,750.00 | - | 19,858,750.00 | 19,858,750.00 |
| | JUMLA | 37,650,000.00 | 40,259,750.00 | 77,909,750.00 | - | 33,838,150.00 | 33,838,150.00 |

KIAMBATISHO NAMBA 6: IDADI YA WAFANYAKAZI WALIOPATIWA MAFUNZO 2005/2006 KWA KILA TAASISI YA WIZARA

(A): MAFUNZO YA MUDA MREFU

| IDARA/TAASISI | SHAHADA YA JUU (PhD) | | SHAHADA YA UZAMILI (MASTERS) | | STASHAHADA YA UZAMILI (PGDIP) | | SHAHADA YA KWANZA | | STASHAHADA YA JUU | | STASHAHADA | | CHETI | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W/KE | W/ME | W/KE | W/ME | W/KE | W/ME | W/KE | W/ME | W/KE | W/ME | W/KE | W/ME | W/KE | W/ME | |
| Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali | - | - | - | - | - | 2 | - | - | 2 | 1 | - | - | 3 | 2 | 10 |
| Mahkama | - | - | - | 1 | - | - | - | - | - | - | - | 2 | - | - | 3 |
| Afisi ya Mwanasheria Mkuu | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | 0 |
| Afisi Kuu Pemba (KUB) | - | - | - | - | - | - | 1 | 1 | - | - | - | - | - | 1 | 3 |
| Idara ya Utawala na Uendeshaji | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | 5 | - | 5 |
| Idara ya Mufti Wa Zanzibar | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | 2 | 1 | 2 |
| Idara ya Kuratibu Shughuli za Utawala Bora | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | 1 | | 1 |
| Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kusimamia Maadili ya Viongozi | - | -- | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | 0 |
| Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali | - | - | - | - | - | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | - | - | 1 | - | 6 |
| Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | 0 |
| Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | 2 | 1 | 3 |
| JUMLA | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 3 | 2 | 2 | 3 | 2 | 0 | 2 | 12 | 6 | 33 |

(B): MAFUNZO YA MUDA MFUPI

| IDARA /TAASISI | IDADI YA WALIOHUDHURIA | | JUMLA |
|---|---|---|---|
| | WANAWAKE | WANAUME | |
| AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI | - | - | - |
| MAHKAMA | - | - | - |
| AFISI YA MWANASHERIA MKUU | 5 | 7 | 12 |
| AFISI KUU PEMBA | - | - | - |
| IDARA YA UTAWALA NA UENDESHAJI | - | - | - |
| AFISI YA MUFTI WA ZANZIBAR | 1 | 1 | 2 |
| IDARA YA KURATIBU SHUGHULI ZA UTAWALA BORA | - | - | - |
| MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA KUSIMAMIA MAADILI YA VIONGOZI | 1 | - | 1 |
| AFISI YA MRAJIS MKUU WA SERIKALI | 1 | 1 | 2 |
| AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA | 1 | 6 | 7 |
| KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA | - | - | - |
| JUMLA KUU | 9 | 15 | 24 |

KIAMBATISHO NAMBA 7: KESI ZA JINAI ZILIZOFUNGULIWA KATIKA MAHKAMA ZA ZANZIBAR KUANZIA JULAI – DISEMBA 2005

| MAHKAMA | KESI ZILIZOFUNGULIWA | KESI ZILIZOTOLEWA UAMUZI | KESI ZINAZOENDELEA |
|---|---|---|---|
| Mahkama za Mwanzo | 667 | 343 | 324 |
| Mahkama za Wilaya | 1984 | 455 | 1529 |
| Mahkama za Mkoa | 322 | 73 | 249 |
| Mahkama Kuu | 1 | - | 1 |
| Mahkama za Watoto | 48 | 13 | 35 |
| **Jumla** | 3,022 | 884 | 2138 |

KIAMBATISHO NAMBA 8: RUFAA ZA JINAI

| MAHKAMA | KESI ZILIZOFUNGULIWA | KESI ZILIZOTOLEWA UAMUZI | KESI ZINAZOENDELEA |
|---|---|---|---|
| R/M/Wilaya | 3 | - | 3 |
| R/M/Mkoa | 24 | 11 | 13 |
| R/M/Mkuu | 2 | 1 | 1 |
| R/M/Rufaa Tanzania | 11 | 2 | 9 |
| Jumla | 40 | 14 | 26 |

KIAMBATISHO NAMBA 9: KESI ZA MADAI ZILIZOFUNGULIWA KATIKA MAHKAMA ZA ZANZIBAR JULAI - DISEMBA 2005

| MAHKAMA | KESI ZILIZOFUNGULIWA | KESI ZILIZOTOLEWA UAMUZI | KESI ZINAZOENDELEA |
|---|---|---|---|
| Mahkama za Mwanzo | 190 | 72 | 118 |
| Mahkama za Wilaya | 11 | - | 11 |
| Mahkama za Mkoa | 21 | 3 | 18 |
| Mahkama kuu | 20 | 2 | 18 |
| Mahkama ya Kadhi wa Wilaya | 566 | 397 | 169 |
| Mahkama za Mirathi | 168 | 77 | 91 |
| Jumla | 976 | 551 | 425 |

KIAMBATISHO NAMBA 10: RUFAA ZA MADAI

| MAHKAMA | KESI ZILIZOFUNGULIWA | KESI ZILIZOTOLEWA UAMUZI | KESI ZINAZOENDELEA |
|---|---|---|---|
| Rufaa/M/ Wilaya | 9 | - | 9 |
| Rufaa M/Mkoa | 33 | 8 | 25 |
| Rufaa/M/Mkuu | 40 | 14 | 26 |
| R/M/Kadhi wa Rufaa | 17 | 10 | 7 |
| R/M/Rufaa Tanzania | - | - | - |
| Jumla | 99 | 32 | 67 |

KIAMBATISHO NAMBA 11: IDADI NA AINA YA KESI ZILIZORIPOTIWA MAHAKAMANI KWA KIPINDI CHA JULAI 2005 HADI MACHI 2006

| AINA ZA MAKOSA | MAHKAMA | | | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| | VUGA | MFENESINI | MWERA | PEMBA | |
| *Madawa ya kulevya* | | *15* | *18* | 2 | 35 |
| *Shambulio la aibu* | | *7* | *1* | | 8 |
| *Kupatikana na silaha* | *6* | | | 1 | 7 |
| *Kupatikana na bangi* | *81* | | | 6 | 86 |
| *Kuua kwa makusudi* | *5* | *1* | | 1 | 7 |
| *Kusababisha kifo kwa uzembe* | *23* | *11* | *3* | | 37 |
| *Kuhatarisha maisha ya mtu* | *1* | | | | 1 |
| *Kughushi* | *1* | | | 2 | 3 |
| *Kutoroka chini ya ulinzi* | *1* | | | | 1 |
| *Kubaka* | *30* | *13* | *24* | 2 | 69 |
| *Kuharibu cha mtu kwa makusudi* | *1* | | | | 1 |
| *kulaghai mtoto kutaka kumuingilia* | *1* | | | | 1 |
| *kumuingilia msichana taahira* | *1* | | | | 1 |
| *Wizi* | *6* | *8* | *1* | | 15 |
| *Wizi wa kutumia nguvu* | | *5* | *7* | 5 | 17 |
| *Fumanizi* | | *2* | | 1 | 3 |
| *Kuua bila ya kukusudia* | | *2* | | 1 | 3 |
| *Shambulio la kuumiza mwili* | *1* | *1* | | | 2 |
| *Kuchoma moto* | | *1* | *6* | 1 | 8 |
| *Kujaribu kunyang'anya* | *2* | | | | 2 |
| *Unyang'anyi* | *21* | | | | 21 |
| *Kuficha kizazi* | *1* | | | | 1 |
| *Kumpa mimba msichana* | | *1* | *4* | | 5 |
| *Kuhatarisha maisha ya mtu* | *1* | | | | 1 |
| *Kujaribu kusababisha kifo* | *1* | | | | 1 |
| *Wizi wa mali ya serikali* | *2* | | | 1 | 3 |
| *Kuvunja jengo na kuiba* | *4* | | | 9 | 13 |
| *Kujipatia fedha kwa udanganyifu* | *6* | | | 1 | 7 |
| *Kuvunja nyumba* | | *1* | | | 1 |
| *Kuvunja nyumba na kuiba* | | | | | |
| *Kujipatia fedha kwa udanganyifu* | | | | 1 | 1 |
| *Kuingia ndani ya nyumba kwa dhamira ya kutenda kosa* | | *2* | | | 2 |
| *Kuvunja jengo* | *4* | *1* | *1* | | 6 |
| *Kumuingilia mnyama* | *1* | | | | 1 |
| *Kutorosha msichana* | *9* | | *2* | 4 | 15 |
| *Kuingilia kinyume cha maumbile* | *2* | | *1* | | 3 |
| *Kumuingilia mtoto wa kiume* | *4* | | | | 4 |
| *Kumkashifu msichana* | *2* | | *1* | | 3 |
| *Uchochezi* | | | | 1 | 1 |
| *Kujaribu kuua* | | *1* | | | 1 |
| *JUMLA* | *218* | *71* | *69* | 39 | 397 |

KIAMBATISHO NAMBA 12: VIZAZI NA VIFO VILIVYOSAJILIWA KIWILAYA

| Wilaya | Vizazi | | | Vifo | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | WME | WKE | JUMLA | WME | WKE | JUMLA |
| Mjini | 3738 | 3937 | 7675 | 410 | 280 | 690 |
| Magharibi | 922 | 857 | 1779 | 30 | 28 | 58 |
| Kusini | 235 | 215 | 450 | 31 | 25 | 56 |
| Kati | 225 | 170 | 395 | 13 | 12 | 25 |
| Kaskazini A | 1037 | 1081 | 2118 | 104 | 73 | 177 |
| Kaskazini B | 450 | 304 | 754 | 25 | 26 | 51 |
| Wete | 900 | 889 | 1789 | 74 | 62 | 136 |
| Chakechake | 972 | 901 | 1873 | 61 | 52 | 113 |
| Mkoani | 793 | 705 | 1498 | 41 | 26 | 67 |
| Micheweni | 623 | 614 | 1237 | 73 | 54 | 127 |
| Jumla | 9895 | 9673 | 19568 | 862 | 638 | 1500 |

KIAMBATISHO NAMBA 13: NYARAKA ZILIZOSAJILIWA

| AINA YA NYARAKA | IDADI YA USAJILI JULAI 2005 - JAN 2006 Unguja | IDADI YA USAJILI JULAI 2005 - JAN 2006 Pemba |
|---|---|---|
| A-1 (REHANI) | 12 | 1 |
| A-2 (MAUZO/URITHI) | 204 | 40 |
| A-3 (WAKFU,HIBA, KIAPO N.K) | 181 | 61 |
| A-4 (KUFUTA REHANI) | 14 | 0 |
| JUMLA | 410 | 102 |

KIAMBATISHO NAMBA 14: ORODHA YA MAHUJAJI WALIOKWENDA HIJJA 05/06 KUPITIA VIKUNDI MBALIMBALI

| No | KIKUNDI | IDADI YA MAHUJAJI | | JUMLA | WALIOTOKEA ZANZIBAR | GHARAMA ZA SAFARI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | WANAUME | WANAWAKE | | | |
| 1. | AHLU –DAAWA HAJJ | 126 | 92 | 218 | 52 | U$D 1600 |
| 2. | JUMUIYA YA ISTIQAMA TZ | 73 | 62 | 135 | 111 | U$D 2000 |
| 3. | ZAHTA | 18 | 12 | 30 | 30 | U$D 2300 |
| 4. | KHIDMAT ISLAMIYA | 63 | 37 | 100 | 20 | U$D 2200 |
| 5. | ZIHATA | 102 | 68 | 170 | 117 | U$D 1650 |
| | Jumla | 382 | 271 | 653 | 330 | |